

TWENDE KWA NANI?



Ndugu Russell. La, hiyo...La. Naam, namaanisha... Ulisema ya kwamba alikuwa mkubwa kidogo, kwa hiyo nikasema...huku juu, lakini sio nje kabisa huku.

² Vema, bila shaka tuna furaha kuwa hapa pamoja na Ndugu Ruddell na kanisa lake tena, usiku wa leo. Nao wana feni, iwapo mna umeme, kwa hiyo jisikieni nyumbani kabisa. Niliketi huko nje kwenye gari na kungojea hata wakati wa kuingia, kwa sababu ni—nilijua kungekuwa na joto. Inaonekana kama, Indiana, tuna majira ya baridi kali halafu tuna kiangazi, kisha tunaingia katika baridi kali moja kwa moja tena.

³ Na kwa hiyo nina furaha maradufu, usiku wa leo, kuwa kwenye mimbara hii pamoja na Ndugu Ruddell, kwa sababu Ndugu Ruddell ni karibu kama mmoja wa wavulana wangu mwenyewe. Ninaweza kukumbuka, miaka mingi iliyopita, wakati mimi na baba yake tulipofanya kazi pamoja. Ndipo wakati mvulana huyu alipokuja, kisha akapata elimu yake, akaenda kwenye Shule ya Mungu ya Biblia, kidogo ilikuwa ni vigumu kwake kuanza. Ilionekana kana kwamba hakutaka kutoka nje, kwa namna fulani. Yeye ni mshamba, mwenye haya. Lakini, hatimaye, akajikakamua, nayo haya ndiyo matunda ya kujikakamua kwake. Nami nafikiri, mimi mwenyewe, kwamba Ndugu Ruddell ndio kwanza anaanza. Huu ni mwanzo tu. Basi ni vigumu kusema hii itapanuka umbali gani. Natumaini itafunika hii misitu yenye giza hapa. Kama ninii...

⁴ Nilikuwa nikimwambia mtu fulani, huko nje, Ndugu Mike Egan. Miaka michache iliyopita, nilikuwa nikiwinda kuchakulo mahali papa hapa. Jinsi ambavyo mambo yanabadilika. Inaonekana kana kwamba ustaarabu ndio kwanza unachukua mamlaka. Hatutakuwa na mahali pa kuwinda kuchakulo wala kuwinda sungura, hata kidogo, kama mahali hapa pakiendelea kupanukia huku. Ni kama tu...

⁵ Miaka michache iliyopita, hapa juu kwenye mahali pa kale ambapo nililelewa, mbona, ingekubidi kutembea maili moja kufika kwa jirani. Sasa, huwezi kumwaga maji nje ya mlango wa nyuma, isipokuwa ungeyamwaga mlangoni pake. Kwa hiyo, kila mtu amesongamana sana.

⁶ Ni vema kuwa hapa. Wala sitawaweka kwa muda mrefu. Ndugu Ruddell ameniomba, wakati mmoja, kuja huku maskanini, kuwaombea wagonjwa.

⁷ Nafikiri, jambo moja linalomfanyia kijana mhudumu kama huyu, tunapokuja na kuwaombea wagonjwa, na hasa sana kama Bwana wetu atatuonyesha tu Utukufu Wake kidogo, italiimarisha kanisa hili changa. Ninawaona baadhi ya marafiki

zangu hapa kutoka maskanini, na baadhi ya wadhamini, na kadhalika. Na sasa, hawa, wengi wa watu hawa wamemwona Bwana akiwaponya wagonjwa. Na, vema, kama Yeye atatufanyia tu tena usiku wa leo, aje jukwaani, katika Utukufu Wake, ita—itaimarisha imani ya watu. I—itawapa tu—tumaini.

⁸ Itamsaidia Ndugu Ruddell, kwa sababu Ndugu Ruddell ameyakinia kuihubiri Injili Kamili. Sasa, angenivunja moyo kama hakufanya hivyo. Nina hakika ingekuwa vivyo hivyo na Bwana. Kwa hiyo, na, halafu, atadumu Nalo kabisa. Basi huenda ikawa mikutano hii midogo itafanya hivyo, kama huu, wakati baadhi yetu wahubiri wa zamani, mnajua, tunaweza kuingia, mbona, inawasaidia hao wavulana wadogo.

⁹ Na sasa, kwa hawa jamaa wa maskanini, nitakuwa huko kesho, lakini nitanini tu. . . Sasa, sitakuwa na wakati wowote wa mapumziko sasa mpaka tarehe kumi na tano Agosti. Ni mkutano tu baada ya mkutano. Kwa hiyo labda, huenda nikaja kwenye shule ya Jumapili, ila si kuhubiri.

¹⁰ Nami nasikitika kusikia, yapata tu saa moja iliyopita, ya kwamba Ndugu Neville, mchungaji wetu, shemeji yake alizikwa leo hii. Nashangaa kama maskani ilijua hilo. Sidhani Ndugu Neville yuko hapa. Nimeangalia kote, kabla sijasema hili. Nashangaa kama walikumbuka kutuma maua huko chini. Kamwe sijui. Ndio kwanza nisikie hilo, dakika chache zilizopita. Billy aliniambia ya kwamba mtu fulani alimwambia ya kwamba shemeji wa Ndugu Neville alizikwa leo. Bila shaka ninasikitika sana kusikia hivyo. Yeye alikuwa ni jamaa yangu wa mbali, kwa ndoa. Nami nasikitika kusikia hivyo, kuondoka kwake.

¹¹ Marafiki zangu wengine wawili wamelala huko chini, usiku wa leo: Dave Wright na Bw. Henson. Hata sikujua walikuwa ni wagonjwa. Wote wawili walifia hospitalini, jana na asubuhi ya leo, nafikiri.

¹² Kwa hiyo, inaonyesha jambo moja, kwamba hatuko hapa kwa muda mrefu sana. Tunasonga mbele moja kwa moja mstarini. Hatujui ni wakati gani Mungu atakapoichukua namba yetu kutoka kwenye rafu ya kadi huko juu. Itatubidi kujibu.

¹³ Kwa hiyo wakati tukiingia kwenye ibada hii, usiku wa leo, ninajua kuna joto, mbaya sana. Lakini hebu na tukumbuke kwamba tunakuja hapa kufanya vizuri tuwezavyo, kumwonyesha Mungu ya kwamba sisi ni waaminifu na tunampenda. Nasi tunataka kila mtu hapa, ambaye hampendi Yeye, apendane Naye usiku wa leo. Nao wote wasiomwamini, tunataka umwamini, usiku wa leo, kwa moyo wako wote. Ili kwamba mkutano huu uwe kitu ambacho kingekuwa alama ya historia, hapa juu kwenye maskani hii, hata ungeweza kurejea nyuma kwenye wakati huu, na kusema, “Usiku huo, Bwana alikuja kwetu na kufanya hivi na hivi.”

14 Kwa hiyo, sasa, kabla hatujaifungua Biblia kwa ajili ya kusomwa kwa Neno. . .

15 Mnaweza kunisikia huko nyuma vizuri, huko nyuma kabisa? Nashangaa, *hapa*, kama mkininii. . . Mnaweza kusikia hayo vizuri? Hiyo ni sawa, *hapa*? Sikuona kutikiswa kwa vichwa vingi mno. Vipi kuhusu hii, hiyo ni afadhali? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Iweke tu moja kwa moja namna *hii*, basi.

16 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Nami nashangaa, katika uchaji wa wakati huu, kungekuwako na mtu yeyote hapa angetaka kukumbukwa katika maombi, kwa kuinua mikono yenu? Mungu awabariki, kila mmoja. Yeye huona na anajua.

17 Baba yetu wa Mbinguni mwenye neema, tunakuja Mbele Zako kwa uchaji, sio tu huku vichwa vyetu vimeimanishwa, bali mioyo yetu imeinamishwa. Kwa kuwa tunatambua ya kwamba imeandikwa katika Neno Lako, ya kwamba, “Walipo wawili au watatu wamekusanyika, nitakuwa miongoni mwao.” Kwa hiyo tuna hakika ya kwamba Wewe uko hapa sasa, kwamba Roho Mtakatifu mkuu anatenda kazi katika jengo hili dogo, kwa sababu ni ahadi ya Mungu.

18 Tunaomba ya kwamba utabariki kukusanyika kwetu usiku wa leo. Libariki kanisa hili dogo na mchungaji wake, na wafanyakazi wenzake wote, washiriki wote. Basi jalia likue na kukua mpaka litakuwa mnara mkubwa sana wa taa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, hata watu watakuja kutoka mbali na karibu, kutembea, kuyaona matendo ya Bwana. Jalia iwe kama lile hekalu la kale, ambamo watu kutoka kote ulimwenguni walikuja kusikia hekima ya Sulemani, na ambapo mambo mengi makuu yalitukia. Na popote tunapokusanyika katika Jina Lake, hapo ndipo mahali pa kukutania, hekalu la Bwana.

19 Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utawaheshimu, usiku wa leo, watumishi Wako, na maombi ambayo tunakuomba, nyimbo tunazoimba. Pia libariki Neno, Bwana. Wakati linapotolewa, jalia kweli lianguke kwenye udongo wenye rutuba. Saa ii hii, Bwana, tunaomba ya kwamba utang’oa kila mwiba, kila shina la uchungu, na kutokuamini kwote, kutoka mioyoni mwa watu; kusudi Neno lipate kuanguka kwenye udongo mzuri, wenye rutuba, ulio na mbolea, hata litawaletea watu hawa matokeo makuu.

20 Wabariki wote walioinua mikono yao. Wewe uliwaona na unajua mahitaji yao. Tujalie hili, Baba, kupitia Jina la Mwanao Mtakatifu, Bwana Yesu, tunaomba. Amina.

21 Sasa, usiku wa leo, ninyi mlio na Biblia zenu, nawatakeni mfungue pamoja nami katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 6, na hebu tuanzie yapata kifungu cha 66, na kusoma nyaraka chache. Yohana Mtakatifu 6:66.

Tangu wakati huo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena.

Basi Yesu akawaambia wale thenashara, Je, ninyi nanyi mwataka kuondoka?

...Simoni Petro akamjibu, Bwana, Twende kwa wanaotafuta anasa. Yeye yuko tu karibu jinsi alivyokuwa wakati alipomwacha Mungu kwenye bustani ya Edeni, naye akaachwa apate kujitegemea. Yeye humwacha tu Mungu waziwazi, na kwenda tu popote atakapo, na kidogo ni mpenda raha kupindukia.

Nasi tunaamini na tuna hakika ya kuwa wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.

²² Ningaliliita somo, ningetaka kulifanya hili: *Twende Kwa Nani?*

²³ Mnajua, watu wa siku hizi wanafanana sana na ilivyokuwa katika siku hiyo. Watu hutembea huku na huku, bila kujua wanakoenda, na inaonekana hawajali hata kidogo. Fursa tu ya kuenda popote watakapo, na—na kwa namna fulani ni watu wanaotafuta anasa. Yeye yuko tu karibu jinsi alivyokuwa wakati alipomwacha Mungu kwenye bustani ya Edeni, naye akaachwa apate kujitegemea. Yeye humwacha tu Mungu waziwazi, na kwenda tu popote atakapo, na kidogo ni mpenda raha kupindukia.

²⁴ Na—naye hajabadilika sana katika fikira zake. Hajabadilika sana katika mawazo yake. Angali anataka dini yake ya jani la mtini, mwajua. Anataka kufanikiwa, yeye mwenyewe, na kujifunika, na kuondoka kama, takriban, ningesema, takriban, kama aliyeridhika, ridhaa ya kujibunia, kama hilo neno linasikika la busara. Anajifanya mwenyewe kuamini ya kwamba ameridhika. Wakati, ndani nafsini mwake, anajua amekosea. Anajua ya kwamba chochote ambacho mwanadamu anapaswa kufanya, kimechafuliwa kwa kuanzia. Wala hawezi kujiokoa mwenyewe zaidi ya vile angeweza kuchukua kamba zake za buti na kuruka hadi mwezini. Hawezi kufanya hivyo. Kujaribu kufanya hivyo, yeye ni kama chui akijaribu kuyaondoa madoa yake kwa kuyaramba. Anaonyesha tu dhambi zake wazi zaidi. Lakini yeye, hata hivyo, hataki kusikiliza. Anatangatanga tu.

²⁵ Lakini, Petro, katika siku hiyo, angeweza kujibu kama wengi wetu usiku wa leo. Alikuwa amepata kitu tofauti. Alikuwa amekutana na Yesu, naye alijua kulikuwako na kitu fulani zaidi ya kutangatanga tu. Mtu yeyote anayepata kukutana na Yesu, kamwe hataki kutangatanga, tena. Kuna jambo fulani linalompata anapokutana na Yesu. Kamwe hawi vivyo hivyo tena. Naye huyu Petro alikuwa amekutana na Yesu, naye alikuwa ameona kitu fulani ndani ya Yesu kilichokuwa tofauti na mtu mwingine yeyote. Kamwe hapakupata kuwepo na mtu kama Yesu. Naye alikuwa ameona kitu hiki kikuu ndani Yake, kilichomfanya kujibu swali hili, “Bwana, twende kwa nani?”

²⁶ Yesu akasema, “Sasa, kama—kama mnataka kwenda pamoja na hao wengine sabini, mko huru, ondokeni tu mwende.”

27 Lakini Petro akasema, “Twende wapi? Tungeweza kwenda kwa nani? Kwa kuwa Wewe pekee unalo Neno la Uzima wa Milele.” Hakuna mwingine aliyekuwa Nalo ila Yeye. Naye Petro alikuwa pamoja Naye kwa muda mrefu kutosha, na alikuwa ameona miujiza Yake na ishara, na maaajabu kutoka kwa Mungu, na kujua kwamba hiyo ilikuwa ni Kweli, kwamba alikuwa na Neno la Uzima wa Milele.

28 Loo, laiti tungaliweza tu kutembea na Yeye muda mrefu kutosha kutambua hilo, ya kwamba Yeye pekee analo Neno la Uzima wa Milele.

29 Sasa Yesu alikuwa na kitu gani ambacho kilikuwa tofauti sana na mtu mwingine yeyote? Kwa nini Yeye alikuwa tofauti na rabi? Rabi alikuwa ni kuhani. Alikuwa ni mwalimu, mwanachuoni. Labda, katika elimu ya ulimwengu, alimshinda Yesu kwa mbali.

30 Hatuna kumbukumbu ya Yesu kuwahi kwenda shuleni, ama kujifunza chochote kutoka kwa mwanadamu. Hakuhitaji hilo. Alikuwa ni Mwana wa Mungu. Ilifunuliwa Kwake, kutoka Mbinguni, jambo la kufanya. Na ufunuo huu wa Kimbinguni ulileta mguso mkubwa sana juu ya wanafunzi hawa, hata Petro akasema, “Twende kwa nani, kulipata Hili?”

31 Na ni halisi tu vivyo hivyo usiku wa leo. Tungeondoka twende wapi kulipata Hili kama hatukuja Kwake?

32 Sasa, nimeandika hapa chini, kwenye kipande cha karatasi, sababu saba, ama mambo saba, ambayo, sababu ambazo imetupasa kuja kwa Yesu. Ninataka kuzungumza juu ya mambo haya saba kwa dakika ishirini ama thelathini tu, kabla hatujawaombea wagonjwa.

33 Mbona, ni kitu gani, alichokuwa nacho Yesu, ambacho kilikuwa tofauti? Ni kwa nini Yeye awe Ndiye pekee?

34 Jambo la kwanza, Yesu alisema, “Mimi ndimi Njia.” Sasa, kuna Mbingu moja tu, na kuna Mungu mmoja, na Njia moja ya kwenda Kule. Hakuna njia nyingi, bali kunayo Njia moja tu ya kufika Huko. Naye Yesu alisema, “Mimi ndimi Njia hiyo.”

35 Sasa, tunajaribu kubuni njia zingine. Tunajaribu kusema zipo njia zingine. Tunayo njia ya kanuni za imani, na tunajaribu kufuata hiyo. Wengi wetu, makanisani, tuna kanuni fulani ya imani ambayo tu—tunakaa nayo. Na hiyo inaweza kuwa ni sawa, kama kifuniko cha jani la mtini.

36 Lakini kama unaenda Mbinguni, inakubidi kupitia kwa njia ya Yesu, kwa kuwa Yeye ndiye Njia. Hakuna njia nyingine inayoweza kuwapo, ya kwenda Mbinguni, ila tu kwa Yesu.

Tuna njia nyingi tunazojiita, “Dhehebu letu.”

Unamwuliza mtu, siku hizi, “Hivi wewe ni Mkristo?”

“Loo, mimi ni Mmethodisti.”

“Wewe ni Mkristo?”

³⁷ “Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mpentekoste, ama Mnazarayo, ama kitu kama hicho.” Hilo silo swali.

³⁸ Kuwa Mkristo, inakubidi kuwa ndani ya Kristo. Na kuna njia moja tu ya kuingia ndani ya Kristo, na hiyo siyo kupitia kwa kanuni za imani wala kupitia kwa makanisa, bali kupitia kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hatuna budi kuzaliwa mara ya pili. Ndipo tunapozaliwa mara ya pili, basi tuko ndani ya Kristo. Basi ikiwa uko ndani ya Kristo, uko kwenye Njia, kwa kuwa Yeye ndiye Njia.

³⁹ Kulikuwako na mtu, wakati mmoja katika Biblia, ambaye Yesu, katika mfano Wake maarufu, alinena habari zake. Kwamba, Yeye alisema kwamba kulikuwako na tajiri mmoja, naye aliandaa chakula cha jioni kwa ajili ya mwanawe, ambacho kilikuwa kinaenda kuwa ni karama ya arusi. Ndipo akawaalika watu waje. Na wakati chakula cha jioni kilipokuwa tayari na kila kitu kikawa tayari kupakuliwa, wageni wote walikuwa wameketi. Basi mezani alipatikana mtu mmoja ambaye hakuwa na vazi la arusi.

⁴⁰ Sasa, watu wengi wanaoisoma Biblia wanalifahamu sana Andiko hili.

⁴¹ Basi huyo mfalme akamwambia jamaa huyu, “Rafiki, mbona uko hapa bila vazi la arusi?” Swali liliulizwa, “Mbona ukaja bila vazi la arusi?”

⁴² Na hivi mliona, Biblia ilisema, ya kwamba, “Hakuwa na la kusema.” Hakuwa na udhuru.

⁴³ Sasa, nimekuwa na majaliwa ya kuwa kwenye maeneo ya Mashariki na kuona arusi za Kimashariki. Hazibadiliki. Mila zile zile, kwa maelfu ya miaka.

⁴⁴ Sasa, wakati kunapopaswa kuwa na karamu ya arusi, kwa heshima ya mtu fulani, bwana arusi hutoa majoho kwa ajili ya watu wote wanaoingia, kwa sababu marafiki zake wanajumuisha maskini, matajiri, na wasiojali. Lakini kila mtu ambaye yeye anamwalika, anapewa mwaliko, na katika mwaliko huu mna jina la bwana arusi juu yake. Basi yeye analeta mwaliko huu mlangoni. Na kuna m—mtumishi anayesimama mlangoni, naye anayo mavazi.

⁴⁵ Kwa hiyo, mtu mmoja anakaribia, amevalia nadhifu sana, ndipo huyo mtumishi anaweka joho la kawaida, juu yake. Mtu wa pili anakuja, yeye ni vivi hivi, hajavalia vibaya sana, bali anapata namna ile ile ya joho ambalo tajiri alipata. Na halafu jamaa anayefuata anakuja, loo, hapana shaka, bali amealikwa kwenye karamu, na ni heshima kubwa kwa rafiki yake, hata ameziosha nguo zake na, loo, akafanya mengi sana kujiandaa, bali amejisumbua tu bure.

46 Basi ndivyo ilivyo, sisi, hakuna kitu tunachoweza kufanya juu yake. Mungu ameleta wokovu wetu kupitia kwa Yesu Kristo. Na sio kwa yale tunayoweza kufanya, au ni mambo mangapi mazuri tunayoweza kufanya. Ambalo, ni sawa, hamna la kusema dhidi yake. “Ila ni kwa neema unaokolewa, kwa njia ya imani.”

47 Ndipo basi mtu huyu maskini anapata joho la aina ile ile ambalo tajiri alipata na huyo mtu mwingine alilopata. Ndipo, wanapoketi mezani, wote wanafanana.

48 Sasa, ni kitu gani kilichompata mtu huyu, ilikuwaje? “Hakuwa na la kusema,” kwa sababu alikuwa amepandia dirishani, ama kuingilia mlango wa pembeni, ama kuingia kwa njia nyingine mbali na ile njia aliyoandaliwa. Basi hakupata joho.

49 Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye Siku ya Hukumu. Zipa njia zingine. Kunazo njia za kanisa. Kunazo njia za kanuni za imani. Kunazo njia za—za mambo mbalimbali. Lakini Yesu alisema, “Mimi ndimi hiyo Njia.” Yohana Mtakatifu 10, Yeye alisema, “Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo.” Nao watu, siku hizi, kama tu walivyokuwa wakati ule, wanakataa tu kuichukua njia hiyo. Wanataka njia yao wenyewe. Wanafikiri ni nzuri vivyo hivyo.

50 Hapa wakati fulani uliopita, ninaamini ilikuwa huko Louisville, kulikuwako na kijana mwanamume. Naye akawa na tatizo kwenye moja ya masikio yake. Vema, akamwendea daktari wake, naye daktari wake akamfanyia uchunguzi kwa majuma kadhaa. Nalo likazidi kuwa vibaya. Hatimaye, huyo daktari akasema, “Sina budi kukutuma kwa mtaalamu.”

51 Basi wakati huyo mtaalamu alipoubaini ugonjwa huo, lilikuwa ni jina kubwa sana la kimatibabu. Ambalo, siamini, kama ningalilijua, kama nigaliweza kulitamka, ingenibidi niandikiwe, na kujizoeza kwa saa moja, kutaja herufi zake. Na halafu msingejua kile nilichosema wakati nilipotaja herufi zake ama kulitamka, maana nisingejua lilikuwa ni kitu gani, kwanza. Lakini sikio lake lilikuwa na tatizo fulani, ambalo lingeuchukua uhai wake. Ndipo akasema, “Ugonjwa huu umeenea sana. Nami sijui mtu yeyote ambaye angeweza kuubaini ugonjwa huu kikamilifu, kuona kama ni kweli hasa ama si kweli, ila mtu mmoja anayeishi huko St. Louis, daktari.”

52 Huyo mvulana akaharakisha kwenda St. Louis. Daktari huyu alikuwa amestaafu na kuhamia New Orleans. Alikuwa Mkusini, kwa hiyo akarudi huko New Orleans. Huyo mvulana akapanda ndege, upesi, akaharakisha kwenda New Orleans. Maskini daktari huyo akauangalia, kasema, “Wameubaini vizuri, mwanangu, nao umeenea sana.”

53 Ndipo kijana huyo akasema, “Daktari, utanifanyia upasuaji?”

54 Akasema, “La, mwanangu. Siwezi kuufanya. Mkono wangu si imara vya kutosha.” Akasema, “Sasa, sijui ila mtu mmoja, ulimwenguni kote, ambaye angeweza kufanya upasuaji huu.” Akasema, “Mtu huyo yuko katika Jiji la New York sasa, akienda kupanda meli aende kwenye likizo ya miezi sita Ulaya. Wala sijui kama hata unaweza kumpata; na hata kama ukimpata, kama hata atafanya huo upasuaji. Ndiye mtu pekee nimjuaye, wa ugonjwa huu usio wa kawaida, angeweza kufanya upasuaji huu. Wala wewe huwezi kungojea. Utakufa katika miezi sita.”

55 Akasema, “Chukua simu. Mpigie. Fanya jambo. Sitaki kufa. Mtafute, kwa vyovyote vile.” Basi hatimaye wakampata huyo daktari naye akakubali kuufanya huo upasuaji.

56 Sasa, wakati kijana huyu alipokuwa akizungumza na huyo daktari mzee, naye akamwambia shida yake ilikuwa ni nini, na kulikuwa na mtu mmoja tu ambaye angeweza kufanya huo upasuaji. Yeye hakumtazama huyo daktari mzee, kama vile watu wengine humtazama mhudumu wakati anapowaambia ya kwamba Yesu ndiye njia pekee ya kuokolewa. Hakumwangualia huyo daktari na kusema, “Hotuba nzuri kweli, daktari. Bila shaka niliyafurahia mazungumzo yako. Nitarudi kuja kukusikiliza, kwenye msimu mwingine.”

57 Sasa, hivyo ndivyo watu huchukulia Ukristo. Lakini laiti ungalitambua tu ya kwamba ni mauti kuikataa Njia hiyo. Hiyo ndiyo sababu Petro alisema, “Twende kwa nani? Kwa kuwa Wewe pekee unao Uzima wa Milele. Wewe Ndiwe pekee, na Njia pekee iliyoandaliwa na Mungu, na hiyo ni Uzima wa Milele.”

58 Sasa, hatuna budi kukumbuka ya kwamba Yeye ndiye Njia. Na kama uko ndani ya Kristo, unaingia ndani ya Kristo kwa kuzaliwa katika Kristo. Sasa hakuna haja ya kuwaambia watu Njia, na Njia ni nini, isipokuwa uwaambie jinsi ya kuingia ndani Yake. Sasa, unazaliwa ndani ya Kristo. Unakuwa sehemu Yake. Unakuwa kiumbe kipya, ama uumbaji mpya, hapo unapozaliwa katika Ufalme wa Mungu. Unakuwa sehemu ya Kristo.

59 Nilipozaliwa katika familia ya Branham, nilifanyika Branham kwa kuzaliwa. Hivyo ndivyo unavyokuwa sehemu ya Kristo. Na jinsi unavyoingia katika Njia, ni kwa Kuzaliwa upya. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo unavyoingia kwenye Njia. Naye Yesu alisema, “Mimi ndimi Njia.” Tungeweza kukaa muda mrefu kwenye hilo.

60 Lakini kitu kingine alichu Yeye, Yeye ni ile Kweli. Hakuna kitu wala mtu mwingine yeyote aliye na Kweli ila Yeye.

61 Loo, ninajua tuna watu wa dini, siku hizi, wanaozunguka na kusema, “Vema, sasa, sisi ndio ile Kweli. Tunayo ile Kweli.” Tunaenda kwa kanisa moja, wao wanasema, “Tunayo ile Kweli.” Tunaenda kwenye kanisa lingine, wanasema, “Kanuni zetu za imani, tunayo ile Kweli.” Tunaenda kwa lingine, “Tunayo ile katekismo ya kale. Tunayo ile Kweli.”

⁶² Yesu alisema Yeye alikuwa ndiye Kweli, kwa hiyo huwezi kuwa na Kweli mpaka umempata Yesu. Unampataje Yeye? Kwa kuzaliwa mara ya pili. Bali huwezi kuwa na ile Kweli mpaka uwe na Yesu.

⁶³ Huwezi kuwa, kuwa katika ile Njia, mpaka uwe ndani ya Yesu. Unaingiaje ndani Yake? “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili mmoja.” Basi uko ndani ya Yesu. Ndipo uko katika ile Njia. Ndipo uko katika ile Kweli. Yesu alisema, “Mimi ndimi Njia, Kweli.”

⁶⁴ Na jambo lingine, jambo la tatu, Yesu, tumekuja Kwake, Yeye ndiye Nuru pekee iliyopo. Hiyo ni kweli. Loo, tunataka kutofautiana na hilo, lakini ni kweli. Yesu ndiye Nuru pekee iliyopo.

Unasema, “Mimi ni Mruseli, Mkampbeli.”

⁶⁵ Hata uwe nani, ni nuru ya bandia. Huenda ukawa katika kanisa la Kiruseli. Huenda ukawa katika kanisa la Kampbeli, ama kanisa lingine la “nuru.” Lakini mpaka utakapoingia ndani ya Yesu, huko katika Nuru. Ungali gizani. Huna Nuru mpaka uingie ndani Yake. Kwa kuwa Yeye ndiye Njia, Kweli, na Nuru, na njia pekee ya kumwendea Mungu. “Hakuna mtu ajaye kwa Baba isipokuwa kwa njia ya Mimi.” Kwa hivyo, huwezi kwenda kwa Mungu, huwezi kwenda Mbinguni.

⁶⁶ Huna budi kuingia kwenye Njia, na Yesu ndiye hiyo Njia. Ndiye Kweli pekee iliyopo. Na Yeye ndiye Nuru pekee, Nuru pekee ya kweli. Nuru pekee ya kweli, iliyodhihirishwa ni Yesu Kristo. Tunayo nuru ya Mormoni. Tunayo nuru ya Kimethodisti. Tunayo nuru ya Kibaptisti. Tunayo nuru ya Kipentekoste. Tuna nuru za kila aina, bali Yesu ndiye Nuru ya kweli. Yeye ndiye Nuru pekee.

⁶⁷ Sisi ndio watoto. Ikiwa tumezaliwa mara ya pili, sisi ndio watoto wa Mchana.

⁶⁸ Watoto wa ulimwengu hutembea gizani. Wanatembea wakati wa usiku. Wanapenda giza. Biblia ilisema, kwamba, “Watu wanapenda, watu wanapenda giza kuliko wanavyoipenda nuru, kwa sababu nuru ingedhihirisha matendo yao.”

⁶⁹ Hebu jua lichomoze, na kila maskini mjusi, kila mdudu wa kale, wadudu wa ufalme wa giza, hutambaa usiku, wataingia chini ya kitu fulani. Hivyo ndivyo wakati Nuru ya Injili inapoanza kuangaza, kila tendo ovyo litajaribu kutambaa chini ya kitu fulani. “Loo,” wanasema, “tuna—tuna nuru, kwa sababu sisi—sisi tunaishi wakati wa usiku.” Kama ukitembea katika nuru wakati wa usiku, unatembea chini ya nuru bandia. Kunayo nuru moja tu ya kweli ya mchana. Hiyo ni nuru ya jua.

⁷⁰ Kuna Nuru moja tu ya kweli ya Kikristo, na hiyo ni Nuru ya Mwana wa Mungu. Yeye ndiye Nuru pekee ya kweli. Naam.

Ndani Yake mna Uzima, ambao, kwa hakika tu kama vile nuru ya jua inavyotoa uhai.

⁷¹ Uhai wote wa mimea hutokea pamoja na nuru ya jua. Mwaka jana ilikuwa hivyo, na jinsi majira za baridi kali zilivyoganda na kadhalika. Lakini mara jua lilipoanza kumulika juu ya dunia, ilikuwaje? Uhai mpya ulianza kutokeza, upya.

⁷² Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani, Bw. Wood huko nyuma. Tulikuwa huko Kentucky. Nilikutana na mtu naye alidhaniwa kuwa ni kafiri. Nilisikia alikuwa ndio kwanza ameaga dunia. Naye, Bw. Wood, alimwendea na kumwomba ikiwa tungeweza kuwinda kuchakulo kwenye eneo lake. Akasema, “Hakika, unaweza kuwinda kuchakulo, Banks. Endelea moja kwa moja.”

Akasema, “Nilikuja pamoja na mchungaji wangu.”

⁷³ Akasema, “Usiniambie umekuwa duni sana, Wood, hata inakubidi kuambatana na mhubiri wakati wote?” Kisha akasema. . .

⁷⁴ Nikatoka kwenye gari nikaelekea huko. Basi palikuwapo na mtofaa, yeye pamoja na maskini muungwana mwingine wameketi chini yake. Ndipo nikaokota tofaa na kuanza kulila. Naye alikuwa akiongea nami. Ndipo nikamta- . . . Ndugu Wood akamtambulisha. Kama . . . Kasema, “Kutana na mchungaji wetu.”

⁷⁵ Nami nikasema, “U hali gani, bwana?” Ndipo tukazungumza kidogo, kisha akaanza kuongea juu ya, vema, ya kwamba kamwe hakuwa amewahi kuhudhuria kanisa, wala hakuja kama alikuwa amepungukiwa na chochote.

Nikasema, “Loo, naam, umepungukiwa.” Nikamwacha azungumze kidogo.

⁷⁶ Ndipo baada ya kitambo kidogo, yeye akasema, “Unajua kulikuwako na mhubiri aliyekuja hapa Campbellsville, ama Acton, mji mdogo, hapa kwenye uwanja wa kupiga kambi wa Methodisti.” Kisha kasema, “Mhubiri huyo kamwe hakupata kuwa humu nchini hapo awali. Ndipo usiku mmoja wakati akiwa huko juu akihubiri, kwenye mkutano wa siku tatu usiku, aliangalia nyuma kwenye umati, akamwona mwanamke ameketi pale, na kumwambia kwamba alikuwa akimwombea dada yake aliyeishi hapa kilimani, akifa kwa kansa. Anasema, ‘Una lesa katika kitabu chako cha mfukoni.’ Kisha kasema, ‘Ichukue lesa hiyo ukaiweke juu ya huyo mwanamke, naye ataponywa.’”

⁷⁷ Kasema, “Asubuhi hiyo, mimi na mke wangu tulikuwa huko juu.” Kisha kasema, “Tulimpindua mwanamke huyo mkongwe katika shuka. Hakuwa ametoka kitandani kwa muda wa miaka miwili, ama zaidi. Kansa ya tumbo. Hata asingeweza kuhifadhi maji tumboni mwake.”

78 Kisha kasema, “Huyo dada akaondoka mkutanoni, na kuondoka usiku huo, akaja akaweka ile lesa juu ya huyo mwanamke.” Kisha kasema, “Kesho yake asubuhi, yeye alikuwa akipika mayai, na nyama ya nguruwe, na kupika kiamshakinywa, na akila.”

79 Basi akasema, “Amekuwa huko juu. Hii ni miaka mitatu ama minne iliyopita, na,” kasema, “angali ni mzima.”

80 Akasema, “Sasa, kama kamwe akija humu nchini tena, nitaenda kumsikiliza.” Kasema, “Kwa sababu, yeye alitoa kitu fulani kilichoonekana kidogo ni zaidi ya lundo la maneno matupu tu ya kusoma. Ilitambulisha kitu ambacho kilikuwa kinaishi na ni hai. Alijuaje kwamba huyo mwanamke aliishi huko juu kilimani?”

81 Nikamwangalia Ndugu Wood na kutikisa kichwa changu. Nami nilikuwa nimesimama pale, nimejaa matope, na damu ya kuchakulo, na kadhalika, kutokana na kuwinda. Kamwe hakuwa na fununu ilikuwa ni mimi huko juu nikihubiri. Kwa hiyo a—alisimama pale kidogo, ama kuketi pale, hasa.

82 Ndipo nikasema, “Bwana, unamaanisha, kama ungeweza kuona jambo fulani lililoonekana kama Mungu, Mungu alifanya kitu fulani cha kimbinguni?”

83 “Loo, naam,” akasema, “hilo lingenifanya niamini.” Nikasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Huu mtofaa una umri gani?”

84 Akasema, “Miaka thelathini na kitu. Niliupanda hapo, hivyo na mwaka fulani.”

Nikasema, “Kila mwaka unaokuja, unatoa matofaa?”

“Naam.”

85 Nikasema, “Hii ni yapata tu katikati ya Agosti. Kamwe hatujawa na mgando mmoja ama kipindi kimoja cha baridi.” Nikasema, “Hatujawa na hali yoyote ya hewa, hata kidogo, ila kiangazi chenye joto. Basi niambie ni kwa nini, inakuwaje, kwamba majani hayo yanapukutika kutoka kwenye mti huo?”

Akasema, “Utomvu umerudi chini ardhini.”

86 Nikasema, “Kama haukurudi, basi mti huo ungekufa kwenye majira ya baridi kali?”

87 “Hiyo ni kweli. Utomvu ukikaa juu mtini, ungeuua. Hauna budi kuingia kwenye mizizi na kujificha.”

88 Nikasema, “Wewe niambie ni kitu gani kinachoufanya utomvu huo, hapa katikati ya kiangazi, ni akili gani inayoutuma chini mizizini, upate kuishi kwenye msimu wa baridi kali, upate kurudi msimu ujao wa kuchipusha majani, kukuletea zao lingine la matofaa. Nitakwambia, ndiye Roho yule yule aliyeniambia niende nikamwambie mwanamke yule aende akaiweke lesa hiyo juu yake. Ni Mungu yule yule.”

Akasema, “Wewe siye yule mhubiri?”

⁸⁹ Nikasema, “Naam, bwana, mimi ndiye.” Nikasema, “Unaona, unaangalia kitu fulani huko nje mkutanoni, lakini Mungu yuko moja kwa moja karibu nawe, kila mahali. Kamwe huwezi kujizuia kuona Hilo. Angalia maumbile.”

⁹⁰ Sasa, watu wengine huenda wakakataa kutembea kwenye mwangaza wa jua. Vipi kama kungekuwako na mtu kama huyo? Ambaye angesema, “Loo, jua haliwaki. La, bwana. Siamini hilo.” Kisha akimbie aingie kwenye chumba chake cha chini. Aseme, “Mimi nitatoka tu giza litakapoingia. Nitakapokuja. . .” Yeye anaukataa usaidizi wa jua. Vema, akifanya hivyo, huo—huo ni ujinga wake tu. Hivyo tu. Jua linawaka. Mtu fulani anakuja dirishani na kupiga makelele, “Toka nje, Yohana. Jua linawaka.”

⁹¹ “Nakataa kuamini upuuzi kama huo. Huo ni ulokole.” Sasa, hakika analikosa joto la jua. Hakika anaikosa miale itoayo uzima linayotoa. Hakika anaukosa uzuri linaloonyesha, na uzima liuletao.

⁹² Hivyo ndivyo, mwanamume ama mwanamke akijaribu kwenda Mbinguni kupitia kanuni ya imani, akijaribu kwenda Mbinguni kupitia kwa kanisa, bila Yesu. Huwezi kwenda. Yeye ndiye Njia, Kweli, na Nuru.

⁹³ Kwa hakika kama vile j-u-a linavyoleta uhai wote wa mimea, M-w-a-n-a hutoa Nuru ya Milele. Yeye pekee yuna Nuru ya Milele. Hiyo ndiyo sababu tunapaswa kuja Kwake. Tutaukosa kupitia kwa kanisa. Tutaukosa kupitia kwa kanuni ya imani. Tunaweza tu kumjia Yeye na kupata Nuru ya Milele. Yeye pekee. Petro alisema, “Wewe Ndiye tu uliye Nayo. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa. Tumekuja Kwako, kuipokea.”

⁹⁴ Sasa, ninyi angalieni wakati mwangaza wa jua unapoanza kuangaza, mbona, hakuna—hakuna mbegu ardhini ila itakayoishi. Haiwezi kujiepusha.

⁹⁵ Hebu tengeneza kinjia cha kando barabarani mwako, ama kupitia njiani mwako, ukitengeneze kwa zege, ukiye upana wa futi nne. Nawe uache jua lianze kuwaka, nazo nyasi zichipuke, unapata nyasi nyingi sana wapi? Moja kwa moja nchani mwake. Ni kitu gani? Ni mizizi hiyo. Huwezi kuuficha uhai kutoka kwenye jua. Jua hilo likianza kuwaka, hiyo mizizi midogo hupenyeza nje urefu wa yadi mia moja, ikibidi, nayo itachipuka. Hiyo ni nyasi iliyokuwa chini ya hicho kinjia cha kando. Hiyo ndiyo iliyokuwa chini mle, nuru inawaka. Ndipo nuru inapowaka, uhai unatokea.

⁹⁶ Na wakati Mwana wa Mungu anapoangaza juu ya moyo, Uzima wa Milele unatokea.

⁹⁷ “Mimi ndimi Njia, Kweli, na Nuru.” Hizo hapo sababu tatu tunazopaswa kujia.

⁹⁸ Ya nne, ni, Yesu ndiye Msingi pekee ulio thabiti na salama ambao chochote kinaweza kujengewa. Hiyo ni kweli. Ndio Msingi pekee unaoweza kujengewa. Misingi mingine yote ni mchanga udidimiao. “Juu ya Kristo Mwamba wenye imara nasimama; sakafu zingine zote ni mchanga unaodidimia.”

⁹⁹ Watu wengi hujenga juu ya utajiri. Wanajaribu kufanya kazi, waone wanaweza kupata pesa ngapi. Wanasema, “Endapo siwezi kuzitumia, watoto wangu wanaweza, nyuma yangu.” Inafanya nini? Inaelekeza kwenye utumwa tena. Unakuwa mtumwa wa pesa zako. Watu wengi labda hawaninii... Haikubidi kuwa milionea kuwa hivyo. Unaweza tu kuwa na tamaa ya pesa, nawe una hatia tu kama milionea. Unaona? Kuna mape-nia wengi tu, kadiri kulivyo na mamilionea, watakaokuwa kuzimuni. Kwa sababu, ni mtazamo wako juu yake, kile Mungu alichokupatia. Sasa, kama ukikijenga juu ya utajiri, kitaporomoka.

¹⁰⁰ Halafu kuna jambo kuu ambalo Marekani hii inajaribu kujengea. Inajaribu kujengea juu ya msingi wa umaarufu. Wasichana wadogo, wavulana wadogo, wanawaangalia, mabingwa wa televisheni, mabingwa wa sinema, wanajaribu kutenda kama wao, kuvalia kama wao, kuwaiga. Linafanya nini? Linaelekeza kwenye maisha yaliyoharibika ya machafuko. Ni mabua na nyasi kavu, ambayo yatateketezwa kwenye ile Hukumu.

¹⁰¹ Yesu ndiye Msingi pekee, Msingi pekee wa hakika. Hiyo ndiyo sababu inatupasa kumjia. Hakuna mtu mwingine aliye na Msingi huo. Utajiri hauna. Umaarufu hauna.

¹⁰² Na, leo hii, tuna misingi mingi sana ya ujenzi. Loo, tunataka...Tunaninii tu...Wamarekani hawawezi kamwe kufanya lolote; Jumapili inawabidi—inawabidi kujenga ua; inawabidi kufanya *hili*. Mnafanya nini? Mnatambua nini? Jengo lenu litalipuliwa vipande-vipande, hivi karibuni sana. Msingi huo ni mchanga unaoporomoka.

¹⁰³ Wengi wetu, tunajenga juu ya elimu. Hata hatuwezi kuwafanya walimu waende shuleni, tunayozungumzia. Sasa, hilo ni sawa. Shule ni sawa, katika mahali pake, bali kamwe haitapachukua mahali pa Kristo. La, bwana. Sasa tuna ninii... Hata hatuwezi kupata walimu. Matineja wetu ni wabaya sana, hata watu hawatajaribu kuwafundisha. Maskini Oswald na—na—na Les, na hao wote, watamfukuza mwalimu kutoka jengoni. Watafanya maandamano. Watagoma. Wataifunga shule. Siwalaumu, wala, mimi nisingekuwa mwalimu wa shule, kama ningaliweza kuiacha.

¹⁰⁴ Lakini tunazungumza kuhusu elimu. Sasa, hiyo ni sawa, elimu. Hatutaki kundi la wasio na elimu, bali tunataka elimu iwe mahali pake. Ila shida yake ni kwamba, siku hizi, tulijaribu kuielimisha mimbara yetu. Nasi tulipofanya hivyo, tuliiondoa ile

Njia. Naye Kristo ndiye Msingi huo pamoja na Njia. Tulipoweka elimu. . . Elimu ni sawa.

¹⁰⁵ Lakini, sikilizeni, mara nyingi, elimu huongoza kwenye pepo wa elimu. Naye pepo huyo wa elimu anakuongoza kwenye ujuaji. Nawe unapofika hapo, basi unakuwa kafiri, na kumkana Kristo. Basi huwezi kujenga juu ya msingi wa elimu.

¹⁰⁶ Wala hatuwezi kujenga juu ya nguvu za kisiasa. Mnasema, "Vema, jamani, ninavutiwa sana. Mimi ni Mdemokrasia. Mimi ni Mripablikani. Mimi ni . . ." Vyama vote viwili vimeoza.

¹⁰⁷ Kuna Msingi mmoja tu. Jenga juu ya Kristo. Taifa hili halihitaji kujenga juu ya msingi mwingine wowote ila Yesu Kristo. Kweli. Hakuna msingi mwingine uliowekwa; hakuna msingi mwingine, unaoweza kuingia Mbinguni kwake. Hakuna msingi mwingine ulio salama, ila Msingi wa Yesu Kristo.

¹⁰⁸ Wakati fulani uliopita, huko New York, nilikuwa nikiendesha pamoja na rafiki yangu, mhudumu. Nami nikasema, "Loo, lile jengo kubwa! Loo!" Nikasema, "Angalia pale. Labda lina orofa hamsini, ama sitini. Loo! Ni mahali pakubwa mno. Jinsi panavyopendeza!" Nikasema, "Vema, hakuna mtu mle."

Akasema, "La, wala hapatakuwapo."

¹⁰⁹ Nikasema, "Kwani kuna nini?" Akanipa makadirio ya kile jengo hilo liligharimu kwa kukadiria, katika mamilioni, kulijenga jengo hilo.

"Vema," nikasema, "kwa nini mtu hakuhamia mle?"

¹¹⁰ Kasema, "Mara lile jengo lilipokaribia kukamilika, upande wote wa nje umeng'arishwa, na kila kitu," kasema, "wakagundua kwamba huo msingi haukuwa sawa. Uliwekwa juu ya namna fulani ya jiwe sabuni, sio jiwe halisi, kwa hiyo jengo hilo likapigwa marufuku. Basi limewahi kutumika tu kwa jambo moja, hilo ni kwa huyo kondrakta kupanda juu yake na kuruka, kujiua."

¹¹¹ Haidhuru upande wa nje unaonekana mzuri jinsi gani, hakuna msingi mwingine ulio wa hakika, ila Msingi wa Yesu Kristo. Yeye ndiye Msingi halisi wa kujengea.

¹¹² Meksiko, jiji la kupendeza; nilikuwa humu ndani, miaka kadhaa iliyopita. Ambako maskini yule mtoto aliyekufa. . .

¹¹³ Nilimchukua mtu fulani kule chini mjini muda mfupi uliopita, mlevi alivyoweza kuwa, nikamwinua. Naye akasema, "Nilikuona ukisimama wakati mmoja, Kasisi, Daktari, ama yeyote yule." Yeye ni Mkatoliki, alisema. Kisha kasema, "Ukamfufua tena, msichana mdogo aliyekufa. Mimi," kasema, "sikuzote nilikuheshimu."

Nikasema, "Unamjua Yesu?"

Akasema, "Mimi ni Mkatoliki."

114 Nikasema, “Kamwe sikukuuliza wewe ni wa kanisa gani. Nilisema, ‘Ulimjua Yesu?’”

115 Ndipo nikamwambia hadithi ya maskini mwanamke huyu mkatoliki aliyesimama huko nje saa tatu asubuhi, akiwa na mtoto mchanga aliyekufa mikononi mwake, mpaka saa nne u nusu usiku huo. Mvua ikinyesha sana, na jinsi ambavyo Bwana alimfufua mtoto huyo mchanga tena. Nisingewaruhusu kulitangaza mpaka baada ya daktari kulitangaza. Kasema, “Huyo mtoto mchanga alikufa.” Akatangaza, “alikufa,” saa tatu asubuhi hiyo. Na huu ni usiku huo saa nne u nusu. Naye maskini mtoto huyo yu hai leo hii, kadri nijuavyo.

116 Sasa, tena katika jiji hilo, ni jiji la kupendeza. Lakini majengo yote yanaanza kuinama nyuma, kwa sababu walivutiwa sana na kupata msanifu majengo wa kisasa, kulifanya jengo hilo la kupendeza na lililong’arishwa. Ambalo, nashuku kama kuna mahali popote ulimwenguni pangeweza kulishinda, katika uzuri. Ila walishindwa kwenda kilindi vya kutosha kufika kwenye mwamba.

117 Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu siku hizi, ewe rafiki. Hiyo ndiyo shida ya Mbaptisti, Mmethodisti, Mpresbiteri, Mpentekoste, Wanazarayo. Inatubidi kuchimba, kama watu binafsi, na tusitegemee makanisa yetu. Hatuna budi kuchimba, sisi wenyewe, mpaka tuufikie Mwamba ule ambao Yesu alisema. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda.” Yeye ndiye Msingi pekee wa kweli, kwa kweli.

118 Halafu, jambo lingine, la tano, itanibidi kusema hivi. Yeye ndiye furaha pekee iliyofanikiwa na ya salama na amani. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kumjia. Loo, ninajua unaweza kucheka kama mpumbavu, ama unaweza kutoka hapa nje na kucheka hata ukaingiwa na mpagao, kwa utani ambao bingwa fulani wa filamu ametoa, ama chochote kile. Ama mtu fulani, huenda kidogo ukanywa kupita kiasi, na kucheka kana kwamba ulikuwa wazimu, bali hilo halileti amani. Hakuna amani nyingine, wala hakuna furaha nyingine, kama kumjia Yesu Kristo.

119 Nimewaona watu wakijifanya. Nimewaona wasichana wakijaribu kujianika huku wamevaa nguo zao mpya, na kujifanya wenye furaha. Hawana. Wanatengeneza tu moto wa kuchorwa. Huwezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa.

120 Mmewaona vijana wanaume wanaojaribu kufikiri misuli yake ilikuwa mikubwa mno hata ungeweza kupigilia msumari wala usiweze kamwe kumgusa, na kisu kilikuwa kimebondeka kwake. Mpe tu miaka michache, naye amegeuka kuwa mzee na kuingia makunyanzi. Hakuna furaha ya Milele nje ya Kristo.

121 Angalieni hapa. Nitaweka...Yeyote wenu hapa, usiku wa leo, mwenye afya kamili, familia yako ina afya kamili, kote kukuzunguka. Vipi kuhusu mama ambaye hayupo hapa?

Unajuaje baba yako hafi sasa? Unajuaje ya kwamba mmoja wa watoto wako hakuuawa, dakika chache zilizopita, mbali na hapa? Unajuaje jambo lingine halijatukia? Unajuaje utatoka humu jengoni usiku wa leo? Huenda ukaanguka katika mshtuko wa moyo. Hujui. Kwa hiyo hakuna furaha ya Milele nje ya Kristo. Hiyo ndiyo sababu hatuna budi kumjia Yeye.

¹²² Unaweza kunywa wiski. Unaweza kupata anasa. Unaweza kupata vitu vya ulimwengu. Lakini hivyo si furaha iliyofanikiwa. Hakuna kitu kinachoweza kutoa amani kama Yeye. Yeye hutoa amani.

“Loo,” unasema, “Ninayo amani.”

¹²³ Kama umepata kuwa na amani halisi, unaye Yesu. Ikiwa huna Yesu; hata hujui amani inamaanisha nini mpaka utakapomjia Yeye.

¹²⁴ Nimewaona watu, wafalme, watawala, watu wakuu, wanariadha, mabingwa wa filamu, na hao wote. Hawana amani. Waangalie. Yatazameni macho yao kwa dakika chache. Wao ni vichaa. Mnaona?

¹²⁵ Hakuna mwanamume, hakuna mwanamke, hakuna mtoto, hakuna mtu anayeweza kuwa na amani nje ya Yesu Kristo. “Amani Yangu nawapa ninyi. Si kama ulimwengu, nawapa ninyi.” Mnaona? Si kama ulimwengu uwapavyo amani, bali Yeye yuna amani ya Milele, amani tulivu. Kama ukiishi, kama ukifa, kama . . . haidhuru kama mvua ikija ama jua liwake, una amani, kwa vyovyote vile.

¹²⁶ Ninaupenda ule wimbo wa kale wa Ndugu Shakarian ambao yeye huimba, jamaa mkubwa, mnene, huimba, “Nina amani kama mto, nina amani kama mto.” Loo, hiyo ni kweli. Unapopata amani, unaye Kristo. Kristo ndiye amani yako. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu hatuna budi kumjia Kristo, tupate amani.

¹²⁷ Sasa, jambo moja zaidi ninataka kusema, kwa ajili ya jambo la sita. Yeye, ama ninii . . . Naam. Jambo la sita, Yeye ndiye mafanikio pekee yadumuyo. Niambieni jambo lolote mnaloweza kupata, mnaloweza kufanikisha, lingekuwa ni la Milele, nje ya Yesu Kristo.

¹²⁸ Kujenga nyumba nzuri. Kupata dola milioni moja. Kuwa mwanamke maarufu sana nchini. Mtu mwenye nguvu sana aliyepata kutembea mitaani. Uishikilie rekodi ya ulimwengu, mpiganaji mkuu, chochote unachotaka kuwa. Angalia kama hutafifia, na kuzorota na kufa. Kweli. Haitachukua ila majua machache kufanya hivyo.

¹²⁹ Kwa hiyo, mafanikio pekee ya Milele yaliyopo, ni Yesu Kristo. Hapo, kama Yeye ndiye mzuri zaidi na bora zaidi tungeweza kupata, hebu—hebu tufanye hayo kuwa mafanikio yetu basi. Hebu tuhakikishe ya kwamba tunampata. Huenda ukawa mhubiri, huenda ukawa mchungaji, huenda ukawa

ni shemasi, huenda ukawa ni mfuasi wa kanisa; lakini endapo huna katika mafanikio yako... Huenda ukafanikiwa kusema, “Sitakoma mpaka niwe mhubiri. Sitakoma mpaka niwe shemasi. Sitakoma mpaka niwe mfuasi wa kanisa.” Mambo hayo yote ni sawa, ya heshima. Lakini, sikiliza hapa, ndugu, usikome kabla hujamfikia Yesu Kristo, la sivyo hujapata mafanikio ya Milele. Kwa kuwa, mchungaji wako, naam, kazi yako ya uchungaji, karibuni itatoweka. Kazi yako kama shemasi itatoweka karibuni. Ufuasi wako wa kanisa utakuwa umefutiliwa mbali zamani kutoka niani mwa watu, muda kidogo tu ujao. Lakini kama umempata Yesu Kristo, basi unao Uzima wa Milele, na huwezi kufa.

¹³⁰ Sasa, mwishowe, ninataka kusema hivi. Hii hapa sababu nyingine inatupasa kumjia Yesu. Yeye Ndiye wa pekee aliye na uhamisho. Ninafurahi sana kwa ajili ya jambo hilo. Loo, hilo linanifanya kujisikia kubarikiwa. Yule pekee anayeweza kuhamisha. Naam, bwana.

¹³¹ Nitakwambia kitu. Shuka uende dukani asubuhi, ama Jumatatu asubuhi, kwa kuwa kesho ni Jumapili. Shuka uende kwenye duka la dawa ukaninunulie dawa ambayo itakufanya mtakatifu sana hata itakuhamisha uingie Utukufuni. Hebu—hebu daktari akufanyie upasuaji, utakaokupa uhamisho kutoka kaburini hata Utukufuni. Hebu kuwa mwerevu na mwenye elimu hata utajua jinsi ya kujenga, kitu kama, mnara mwingine wa Babeli; utaishia vile vile. Tafuta kujua. Jaribu kupitia njia nyingine, upate kujua.

¹³² Ni wale tu walio katika Kristo ambao Mungu atawaleta pamoja Naye. Uhamisho pekee unaoweza kufanywa kutoka duniani hadi Utukufuni ni kupitia kwa Yesu Kristo. Yeye Ndiye uhamisho wa pekee, njia pekee ya kuhamishwa. Huwezi kuununua. Huwezi. Huwezi kuufanyia kazi. Huna budi kuupokea. Ni zawadi kwako. Uhamisho wa Mungu, kukuchukua.

¹³³ Shuka hapa chini ukaninunulie dawa itakayokubadilisha, kutoka mzee mwanamume ama mwanamke, urudi kuwa kijana mwanamume ama mwanamke. Tafuta kujua kama unaweza kuinunua. Kamwe hutaweza. Kamwe haitakuwako, katika milki ya tiba. Kamwe haitakuwako katika milki yoyote nje ya Yesu Kristo.

¹³⁴ Lakini Yeye alisema hivi, “Yeye aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku za mwisho, kumhamisha, kumpeleka Utukufuni.” “Kama mwili huu ulio wa dunia hii ukiharibika, maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibika, tunayo moja inayongojea.” Kuhamishwa, kubadilisha makazi, kwenda kutoka mahali pamoja hadi pengine. Yeye Ndiye pekee aliye na Uzima wa Milele. Yeye Ndiye pekee aliye na furaha.

¹³⁵ Naweza niseme hivi, pia? Yeye ndiye pekee... Ndani Yake ndimo mahali pekee unapoweza kwenda, ambapo unaweza kumwona. Mahali pekee ambapo kamwe utaweza kumfahamu, ni hapo utakapoingia ndani Yake. Huna budi kuingia ndani Yake, upate kuifahamu. La sivyo, utaninii tu—utashangaa tu na kupigapiga kichwa chako huku na huku. Utabahatisha. Nawe utaninii... Itakuwa ni fumbo kwako. Kamwe hutalielewa.

¹³⁶ Hiyo ndiyo sababu Wayahudi hao, katika siku hizo, walisema, “Mbona, jamaa huyu ni Beelizebuli. Jamaa huyu ni *hiki, kile, na kinginecho*.” Kamwe hawakumjia. Kamwe hawakumkubali Yeye kama Njia. Kamwe hawakumkubali Yeye kama Kweli, kama Nuru, kama Msingi, kama wa Kwanza, kama wa Mwisho, kama Alfa, Omega, mambo haya mengine yote aliyo Yeye. Yeye ni Yote kwa Yote. Hiyo ndiyo sababu wasingeweza kumwelewa wakati walipomwona Yeye.

¹³⁷ Filipo akatokea, ambaye alienda kule na kumpata Nathanaeli, akamleta Nathanaeli. Naye Nathanaeli, Yesu... akaenda Mbele za—za Yesu. Wakati Nathanaeli alipokuja mbele za Yesu, hasa, Yesu alimtaazama na kusema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Kasema, “Rabi, ulinijua lini Wewe?”

¹³⁸ Kasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Ninii...

¹³⁹ Wahubiri wakisimama pale, makuhani, wakasema, “Mtu huyu ni Beelizebuli. Yeye yuna ibilisi ndani Yake. Ni mpiga ramli.”

¹⁴⁰ Yesu akasema, “Ukisema hivyo dhidi Yangu, nitakusamehe. Lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja, kufanya jambo lile lile, wala neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu ama ulimwengu ule ujao.”

¹⁴¹ “Mwawezaje,” Yeye akasema, “mwawezaje kunihukumu Mimi, wakati neno lenu wenyewe linasema ninyi ni ‘miungu’? Na kama waliitwa ‘miungu’ ambao walijiliwa na Neno la Mungu, mwawezaje kunihukumu ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?”

¹⁴² “Kama mngalimjua Baba Yangu, mngalinijua Mimi pia.” Hiyo ni kweli. Akasema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu.” Hakuna mtu atakayemfahamu Mungu, isipokuwa Kristo, wengu mkubali Kristo. Huwezi kuelewa uponyaji wa Kiungu.

¹⁴³ Mbona, mtu fulani anasema, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Maskini mchungaji hapa huenda akalihubiri.

¹⁴⁴ Baadhi yenu huenda mkakwaruza kichwa chenu na kusema, “Aha, siamini jambo hilo.” Mnaona? Wewe huko katika hali ya kuliadini. Likubali tu, kwa imani, ndipo basi utalionga.

¹⁴⁵ Yesu alisema, “Muda kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, hiyo ni, utaratibu wa ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona Mimi; ninyi, mwaminio, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Hata nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Nitaondoka, kisha nitarudi tena na niwe pamoja nanyi.”

¹⁴⁶ Nikodemo aliuliza lile swali. “Ninawezaje kuzaliwa mara ya pili. Mimi ni mzee. Niingie tumboni mwa mama yangu mara ya pili?”

¹⁴⁷ Akasema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona Ufalme wa Mungu.” Sasa, fasiri hiyo pale kweli ni “kuufahamu,” kuufahamu Ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu uko ndani yenu, kwa hiyo usingeweza kuuona hasa, isipokuwa uuone ukitenda kazi. Lakini njia pekee utakayoweza kuufahamu, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili, umejazwa na Roho wa Mungu, basi uko ndani ya Kristo. Ndipo wakati ukiwa ndani ya Kristo, Roho Mtakatifu aliyeandika Biblia, ambaye alimthibitisha Kristo, yuko ndani yako, kujitambua Mwenyewe. Amina. Hiyo ndiyo sababu huna budi kumjia.

¹⁴⁸ Hiyo ndiyo shida ya Marekani siku hizi. Mikutano hii imeenea nchini, kutoka mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini. Hiyo ndiyo sababu bomu la atomiki, limepandwa huko ng’ambo kwa ajili ya taifa hili. Hiyo ndiyo sababu maangamizi yamekaribia. Ni kwa sababu kazi za Mungu zimedhihirishwa, nao watu wakaondoka pasipo kuzikubali, kwa sababu hawamtaki. Wanamwonea aibu. Loo, hawalionei aibu kanisa lao. Hawaionei aibu dini yao. Lakini wanamwonea Yesu Kristo aibu.

¹⁴⁹ Wakati mitume walipoliacha kanisa lao, na kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kwenye Pentekoste, akawafanya kuyumbayumba kama walevi, kunena kwa lugha nyingine, na kupiga makelele, na kuendelea, na kuwaponya wagonjwa, na kadhalika. Nao wakaitwa kundi la—la—la wasiojua kusoma wala kuandika, wasio na elimu. Biblia ilisema “Walikuwa wasio na elimu wala maarifa. Lakini walitambua kwamba walikuwa pamoja na Yesu,” kwa sababu walitenda vile vile alivyotenda. Walijua ya kwamba uhai Wake ulikuwa ndani yao, kwa sababu walikuwa wakifanya kazi alizofanya Yeye.

¹⁵⁰ Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:7, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Haya basi. Hiyo ndiyo sababu inatubidi kumjia Kristo leo hii.

¹⁵¹ Ninaamini Kristo yuaja karibuni. Ninaamini tuko mwishoni mwa safari. Ninaamini mataifa yanavunjika. Ninaamini wakati wa mwisho umekaribia. Ninajua umekaribia. Kwa kweli, ninajua kabisa umekaribia. Nitasonga mbele zaidi, na kusema, “Ninaamini ya kwamba ninajua hilo.” Tuko mwishoni mwa

safari. Kwamba ni siku ngapi, ni miaka mingapi, ama majuma, sijui mimi. Hakuna mtu ajuaye. Si hata Yesu; Yeye alisema, “Mungu anajua hilo, pekee.” Sijui itakuwa lini, itakuwa saa ngapi. Lakini ninajua kwamba ni karibuni, kwa kuwa haya ndiyo mambo yanayopaswa kutendeka kabla tu ya Kurudi Kwake.

¹⁵² Hebu nikushawishi, usiku wa leo, rafiki yangu uliye nje ya Kristo. Kama unataka Msingi imara, Njia, Kweli, na Nuru, mkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako binafsi na kujazwa na Roho Wake. Ndipo wakati Roho Wake akianza kutenda kazi, utamjua Roho Wake.

Hiyo ndiyo iliyokuwa shida yao wakati ule. Walimwona.

¹⁵³ Yule mwanamke kisimani, yeye alijua zaidi kumhusu Mungu kuliko nusu ya wahubiri walivyojua, wa siku hizo. Mbona, mara alipomwona Yeye, yeye... Yeye alionekana kama Myahudi wa kawaida, mtu tu wa kawaida. Ndipo Yeye akamwambia mwanamke huyo, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹⁵⁴ Mwanamke huyo akasema, “Mbona, si kawaida kwenu ninyi Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho.”

¹⁵⁵ Akasema, “Lakini kama ungejua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ningekupa Maji usije hapa kuteka.”

¹⁵⁶ Aliendelea kuzungumza naye hata akampambanua, akamshika, iliyokuwa shida yake. Kila mmoja wetu anajua shida ilikuwa ni nini. Sisi Wamarekani tunaamini ya kwamba alikuwa ni mzinzi. Alikuwa na waume watano, huku akiishi na wa sita.

Kwa hiyo akasema, “Nenda kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

¹⁵⁷ Akasema, “Umesema kweli. Ume kuwa na watano, naye unayeishi naye siye mume wako. Umesema kweli.”

¹⁵⁸ Akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua, ajapo Masihi, atajitambulisha Mwenyewe kwetu hivyo. Tunajua ya kwamba Yeye atatwambia mambo haya.”

Akasema, “Mimi Ndiye, ninayesema nawe.”

¹⁵⁹ Akauacha mtungi wa maji, naye huyo akaingia mjini. Alikuwa amefanya nini? Alikuwa amekubali. Alikuwa ameukubali, ule ufunuo ulipomjia. Akakimbia mjini na kusema, “Njoni, mumwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Alikuwa ameukubali. Haya basi.

¹⁶⁰ Wakati, Mafarisayo na Masadukayo walipogeuka, wakasema, “Yeye ni Beelizebuli. Hatutakuwa na uhusiano

wowote Naye. Kwa sababu di-...” Walikuwa na msingi. Walikuwa na njia. Walikuwa na njia.

¹⁶¹ Biblia ilisema, “Iko njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu; mwisho wake ni njia ya mauti.” Kwa hiyo, usipitie njia hiyo ione kanayo kuwa sawa.

¹⁶² Njoo kwa Kristo, mkubali Yesu kama Mwokozi wako, kisha ujazwe na Roho Mtakatifu. Ndipo, wakati Roho Mtakatifu anapoanza kutenda kazi miongoni mwenu, mtamtambua.

¹⁶³ Hiyo ndiyo njia ya kuponywa, kujua mponyaji ni nani. Yesu Kristo ndiye mponya. Angetendaje kama angalikuja hapa, usiku wa leo, kuwaponya? Angetenda vile vile alivyotenda kule nyuma.

¹⁶⁴ Mwanamke mmoja alijisukumiza kwenye umati na kuligusa vazi Lake. Akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?” Ndipo kila mtu akasimama. Naye akaangalia kote hata akampata. Ndipo akamwambia kwamba alikuwa na ugonjwa wa kutokwa damu, kisha kasema, “Imani yako imekuokoa.”

¹⁶⁵ Huyu alikuwa ni Yesu jana. Huyu ni Yesu leo, endapo Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Huwezi kuamini hilo mpaka umempokea Kristo ndani yako, kisha Yeye anashuhudia, Mwenyewe, kwamba ni Yeye. Mnaona ninalomaanisha? Hiyo ndiyo njia ya kumpata, ni kumpokea Yeye.

¹⁶⁶ Hizo hapo sababu saba kwa nini inatupasa kumpokea sasa. Hatuwezi kumwendea mwingine. “Wewe tu.” Huwezi kwenda kanisani na kumpata Huyu. Sijui dhehebu unaloweza kuliendea na kumpata. Si—sina neno dhidi ya dhehebu. Lakini watu wengi wanadhania tu, kwa sababu ni washiriki wa kanisa, hivyo tu ndiyo inavyowapasa kufanya. Inakubidi kumjia Yesu. Yeye ndiye Njia, sio kanisa. Yeye ndiye Kweli, sio kanisa. Yeye ni Nuru, sio kanisa. Yeye ni Msingi, sio msingi wa kanisa. Yeye ni furaha ya Milele, Uzima wa Milele, Mafanikio pekee yadumuyo, Uhamisho pekee. Njia pekee ya kumjua Mungu, Njia pekee ya kuuona Ufunuo, Njia pekee ya kuponywa, ni kumjia Yeye. Huna budi kumjia Yeye, na kumtambua, kumwamini.

¹⁶⁷ Sasa unasema, “Vema, Ndugu Branham, sijawahi kuona kazi kama hizo zikifanywa.”

¹⁶⁸ Vema, natumaini utazona. Natumaini utaona hizo. Mkutano sasa unakaribia tu kuanza. Ninawatakeni hapa, ambao wanataka kumpata, kumjua, wangeomba wapate kumjua. Ni wangapi wangetaka kumjua kusudi mweze kumtambua kama Roho Wake akija mkutanoni? Inua mkono wako. Sema, “Ningetaka kumjua kwa njia ambayo ningemtambua.” Nawashukuru.

¹⁶⁹ Ungemtambua jinsi gani? Kwa sababu kwamba angefanya kazi zile zile alizofanya wakati alipokuwa hapa duniani. Sasa, Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema nini?

¹⁷⁰ Alipitia kwenye Birika la Bethesda, kule, kundi kubwa la watu, viwete na vilema. Yesu alipitia karibu na hao elfu mbili, ama zaidi, watu, akapitia karibu nao. Akamwona mtu amelala kwenye kitanda cha wagonjwa. Kwa kuwa, Yeye alijua, unaona; alikuwa amemwona, awali. Alishakuwa hapo miaka hii yote. Naye akasema . . . Hakuwa kiwete, angeweza kutembea. Akasema, “Wataka kuwa mzima?”

¹⁷¹ Akasema, “Sina mtu wa kunitia majini. Ninapokuja mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu, anayeweza kutembea haraka zaidi, kuingia kwanza.” Akasema, “Wakati nikija, mtu mwingine anashuka mbele yangu.”

¹⁷² Akasema, “Jitwike godoro lako uende nyumbani mwako.” Huyu mtu akatwaa godoro lake akaenda zake.

¹⁷³ Akaondoka akawaacha hapo. Sasa, hilo halikusikika kuwa zuri sana, sivyo? Lakini huyo alikukwa ni Yesu. Moyoni, “Kwa nini?”

¹⁷⁴ Sasa, kama mtaendelea tu kusoma kifungu kingine, kifungu cha 19, mtaelewa ni kwa nini Yeye alifanya hivyo. Walipomswali, Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya lolote Mwenyewe. Ila lile amwonalo Baba akilitenda, hilo atenda Mwana.” Mnaliona? “Jinsi Baba, atendavyo kazi, ndivyo Mimi hutenda kazi.” Kwa maneno mengine, “Baba hunionyesha ono. Ninaona yale anayoniambia kufanya, nami ni—nitasema tu yale aniambiayo kusema. Nitafanya yale tu Yeye aniambiayo Mimi nifanye.”

¹⁷⁵ Vema, huo ndio Msingi. Hiyo ndiyo Kweli. Hiyo ndiyo Njia. Hiyo ndiyo Nuru. Haleluya! Huyu ni Yesu.

Unasema, “Sijawahi kumwona.”

¹⁷⁶ Naomba niseme hili, katika kufunga. Majuma machache yaliyopita, huko chini Florida, karibu na ghuba la Meksiko, mahali fulani huko chini, ama huko chini kwenye Funguo mahali fulani. Kulikuwako na da—daktari, nafikiri alikuwako, aliyeshuka kwenda kuvua samaki. Na yeye—yeye akamkodi kiongozi mzee aliyedhaniwa kuwa ni kiongozi mzuri sana, ambaye angejua jinsi ya kumwingiza na kumtoa majini. Basi huyo mzee kiongozi aliingia tu kwenye mashua, na kuondoka, akaenda ndani kidogo kwa matanga yake, kisha akangojea kidogo. Wala hakukuwa kumepambazuka bado.

¹⁷⁷ Naye—naye jamaa huyo akaanza kuhisi hizo pepo za kiajabu, kama vile zinavyokuja baharini kila asubuhi, zikizunguka. Akasema, “Aisee,” akaanza kuwazia, “Tunaelea huku nje baharini. Wimbi linatusukuma huko nje.” Aliiona hiyo mashua, ilionekana kana kwamba walikuwa wakisogea. Akasema, aliwazia, “Sitaki kuzungumza na huyo kiongozi, bali afadhali—afadhali niseme jambo fulani.” Akaingia wazimu. Akasema, “Aisee, bwana, tunaelea baharini, sivyo?”

“Loo,” akasema, “Sidhani.” Mtulivu, mnyamavu.

¹⁷⁸ Kitambo kidogo, akaiona ile mashua, ingali inajongea, ukungu na giza. Akasema, “Tunaelea huko baharini. Fanya jambo. Wewe ndiwe kiongozi. Fanya jambo. Harakisha. Tunaenda baharini. Turudie njia gani?”

¹⁷⁹ Yule mzee kiongozi, mtulivu tu alivyoweza kuwa, aliketi pale, na kusema, “Vema, ngoja tu muda mfupi, itakuwa nuru, ndipo tutajua mahali tulipo.”

¹⁸⁰ Ngoja tu kidogo. Nuru ya kweli ya Mungu na ilianguzie jengo hili, usiku wa leo. Ndipo utaona mahali ulipo. Utaona njia ya kuendea, baada ya hapo.

Na tuombe.

¹⁸¹ Baba wa Mbinguni, imesemwa katika Maandiko, “Mimi ndimi Njia, Kweli, na Nuru. Hakuna mtu ajaye kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi. Mimi ndimi mlango wa zizi la kondoo.” “MIMI NDIMI, MIMI NDIMI, MIMI NDIMI,” kuendelea na kuendelea, mpaka, hatimaye, Wewe unaishia, kusema, “MIMI NDIMI AMBAYE NIKO.” Huyo “MIMI NIKO” hakuwa jana wala kesho. Yupo sikuzote, yeye yule, “MIMI NIKO.” Katika kila wakati, katika kila kizazi, kote katika Umilele, angali, “MIMI NIKO.” Sasa, Wewe ungali ni yule “MIMI NIKO” mkuu, sio “Nilikuwa” wala “nitakuwa.” Hata hivyo, Wewe ulikuwa, na utakuwa. Lakini, hata hivyo, Wewe upo siku zote, “MIMI NIKO.”

¹⁸² Si ajabu mtume alisema, “Twende kwa nani, Bwana? Twende kwa nani? Tunakuona Wewe ukiyafanya mambo haya. Tunajua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kufanya mambo haya, Mungu asipokuwa pamoja naye.”

¹⁸³ Nikodemo alitangaza vivyo hivyo, “Rabi, twajua ya kuwa Wewe ni Mwalimu uliyetoka kwa Mungu. Tunajua hilo. Sisi Mafarisayo, sisi wafuasi wa kanisa, tunajua hilo. Hatuwezi kulikubali. Tutafukuzwa kanisani. Lakini tunajua ya kwamba Wewe ni Mwalimu uliyetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu awezaye kuzifanya kazi uzifanyazo Wewe, isipokuwa Mungu alikuwa pamoja naye.”

¹⁸⁴ Kweli, Bwana, ndivyo ilivyo siku hizi. Wewe ni Msingi ule ule; Njia ile ile, Kweli ile ile, Nuru ile ile. Msingi ule ule! Wewe ni furaha ile ile. Wewe ni uhamisho ule ule. Wewe ni yeye yule kwa hayo yote. Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele; Yeye yule aiujaye siri ya moyo. Yule yule jana, leo, na hata milele; mponya yule yule, Mwokozi yule yule.

¹⁸⁵ Mungu, huenda kukawa na wenye dhambi hapa. Mikono ishirini ama thelathini iliinuliwa, muda mfupi uliopita, nilipouliza ni nani angetaka kukuona Wewe. Ninawaweka kando, muda kidogo zaidi, juu ya tamshi langu la mwisho, “Ngoja mpaka Mwana atakapoangaza, ndipo utaona mahali ulipo. Usiingie kichaa. Usitoroke kanisa. Usiwe, useme, ‘Ni

joto sana kuketi hapa tena.' Lakini hebu tungoje kidogo. Acha Mwana aangaze. Acha Nuru ichomoze. Hebu Yesu ajitokeze jukwaani na kutenda na kufanya kama yale aliyofanya hapa wakati Yeye alipokuwa duniani, ndipo tutakapooni njia ya kupitia." Tujalie, Baba. Tunaomba haya katika Jina la Yesu na kwa utukufu Wake. Amina.

Ninajua kuna joto. Hatuna muda mwingi sana.

¹⁸⁶ Ni wangapi wanaoamini ya kwamba matamshi hayo ni ya kweli? Hakuna njia nyingine yoyote ya kugeukia. Hakuna njia nyingine.

"Vema, unawezaje kuwa na hakika?"

¹⁸⁷ Nimelihukumu kanisa, kama dhehebu. Nimehukumu msingi lililojengwa juu yake, juu ya fundisho la maaskofu na kadhalika, "Wenye mfano wa utauwa, huku wakikana Nguvu zake." Kwa sababu, hawaamini katika uponyaji wa Kiungu. Hawaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hawaamini katika Mafundisho ya Injili yote. Madhehebu yao, Wapentekoste, yanaenda mbali viyvo hivyo. Hiyo ni kweli. Nazarayo, Pilgrim Holiness, wamechukuliwa na mkondo, kwa sababu wameanza kukubali fundisho la mwanadamu, dini ya jani la mtini. Mwanadamu, akitembea polepole, "Twende wapi?" Utakuwa kama wale sabini, ambao wangeondoka?

¹⁸⁸ Ama, utakuwa kama Petro, usiku wa leo? Useme, "Bwana, twende kwa nani? Tumwendee nani mwingine? Tumeona kwamba Wewe unalo Neno la Uzima wa Milele. Wewe Ndiwe pekee uliye Nalo."

¹⁸⁹ Na Yesu Ndiye pekee aliyeishika nafsi yako mkononi Mwake. Kanisa lako haliwezi kukusaidia. Kristo anakusaidia.

¹⁹⁰ Ni wapi unakoweza kupata...ama kuamini au kuona Msingi unaoweza kufanikisha kitu chochote baada ya mauti? Kanisa linaweza kukufanyia kitu gani baada ya mauti? Kanisa linaweza kukufanyia nini wakati madaktari wamekukatalia mbali? Mtu yeyote anaweza kukufanyia nini wakati sayansi ya tiba imekukatia tamaa, umeliwa na kansa? Hakuna kitu.

¹⁹¹ Ila kunao Msingi. Kuna Mmoja. Ipo Njia. Ipo Nuru. Yupo Mungu. Kuna mponya. Kuna Mwokozi. Kuna Mmoja aliyetukuzwa, Naye yuko miongoni mwetu usiku wa leo, kwa sababu aliahidi atakuwako.

¹⁹² Naye akasema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa miongoni mwao. Kazi nizifanyazo Mimi watazifanya pia. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu," huo ni kanisa tu, walio nje, "hawataniona Mimi tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi..." Na mtu yeyote aliyewahi kwenda kwenye shule ya sekondari anajua kwamba "Mimi" ni kiwakilishi nafsi. Mnaona? "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dhari. Na kazi nizifanyazo ninyi

nanyi pia mtazifanya.” Ni kazi gani alizofanya? Kama vile Baba alivyomwonyesha.

¹⁹³ Hiyo ndiyo sababu nilisema katika tamshi langu la mwisho, “Ngojeni.” Sijawahubiria bure. Endapo Yesu hatafanya nisemayo, yale Biblia iliyosema alifanya, yale niliyonukuu, ninyi... Maandiko aliyoyafanya, basi nimewaambia uongo; basi Biblia imekosea; basi hima twendeni tukaitafute dini ya Kiislamu, hebu tumtafute Budha, dini nyingine iliyo ya kweli.

¹⁹⁴ Hebu niwaambie sasa hivi, ndugu, kabla hujaanza, kunayo Njia moja tu, Ukweli mmoja pekee. Kuna dini moja pekee iliyopo, inayoweza kuthibitisha ya kwamba Mwanzilishi wao alifufuka katika wafu na yu hai milele, amina, hilo ndilo Kanisa la Mungu aliye hai. Limefanyizwa kwa Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, na wowote wale, Nazarayo, Pilgrim Holiness, Wapentekoste. Kila mwanadamu aliyezaliwa katika Ufalme wa Mungu, ambaye amempokea Yesu Kristo, amejengwa juu ya Msingi huo wala kamwe hawezi kufa, anapumzikia tumaini hilo la Milele. Ingawa huenda wakatupa mavumbi juu ya jeneza lako, katika juma moja kuanzia sasa, hata hivyo halitakusumbua hata kidogo. Unatoka tu kwenye jengo hili la kale, kuingia lile jipya, hivyo tu. Yeye atakufufua katika siku ya mwisho.

¹⁹⁵ Yesu Kristo ndiye mahali pekee pa kugeukia. Ninamgeukia Yeye, kwa moyo wangu wote, kwa nguvu zangu zote. Kama vile ningalikuwa kama nilikuwa na laki tano, kama tulivyofanya huko Bombay. Hapa katika kanisa hili dogo, usiku wa leo, la watu mia moja na hamsini, ama kitu kama hicho, labda sio wengi hivyo. Vile vile, kujituliza juu Yake, apate kujifunua Mwenyewe kwa njia fulani, usiku wa leo, hilo litawafanya kuelewa ya kwamba Yeye yupo hapa.

¹⁹⁶ Kadi za maombi? Ulisambaza zozote? [Mtu fulani anasema, “Naam.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Ulisema ulisambaza ngapi? [“Kama ishirini.”] Ndugu Ruddell, nilikuwa nikitarajia, usiku wa leo, kweli. Lakini imekuwa ni joto sana, watu wangesongamana na kujaa, na kujaa hapa ndani, na ka—kadhalika. Lakini ni—ni kwamba, nadhani, wao... Kama nilivyofanya, kwanza. Nilitaka kwenda kumchukua mke wangu, nami nikapitia hapa, kuona kama ilikuwa... ni wangapi waliokuwa hapa, nami nikaona lilikuwa limejaa, nikarudi tu humu. Mnaona? Nikaja, nikageuka, nikarudi.

¹⁹⁷ Sasa, kuna joto. Lakini, loo... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Wachache tu, halafu labda tutapata wengine zaidi, wengine zaidi, na kuwaombea.

¹⁹⁸ Sasa, sisemi Bwana atafanya lolote kubwa sana kwa ajili yetu. Labda atafanya. Labda hatafanya. Sijui mimi.

¹⁹⁹ Sasa, ipi, ulianzia moja? [Mtu fulani anasema, “Moja.”—Mh.] Moja. Vema. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja?

Unaweza tu kuinua mkono wako. Mtu fulani aliye na kadi ya maombi namba moja. [Mtu fulani anasema jambo fulani.] Una hakika na hilo? Namba moja? ["Endelea. Amesimama huko nyuma."] Loo, samahani. Vema, mama, njoo papa hapa.

²⁰⁰ Namba mbili, ni nani aliye na namba mbili? Kadi ya maombi namba mbili, naomba uinue mkono wako. Msichana mdogo. . . Loo, sa—samahani. Kadi ya maombi namba mbili, tafadhali inua mkono wako. Sawa.

²⁰¹ Mnamaanisha kadi ya maombi namba mbili haipo hapa ndani? Huyu mama. Vema. Njoo papa hapa, mama. Papa hapa.

²⁰² Namba tatu. Angalieni upesi, sasa, huenda ikawa ni mtu aliye kiziwi, ama mtu asiyeweza kusimama. Namba tatu, inua mkono wako, tafadhali. Kadi ya maombi namba tatu. Vema, bwana. Ninamjua mtu huyu. Vema.

²⁰³ Namba nne, inua mkono wako. Kadi ya maombi namba nne. Mtu fulani aliye na namba nne, tafadhali. Mama huyu hapa. Ninaamini ninamjua mama huyu. Sijakosea. Nafikiri namjua. Namba nne.

Namba tano. Huko nyuma kabisa. Vema.

Namba sita. Kadi ya maombi namba sita. Vema.

Namba saba. Kadi ya maombi namba saba, huyo bwana anayekuja.

Namba nane.

²⁰⁴ Billy, naomba ushuke uende ukawapange, kusudi mwe na mahali pa kusimama, au jambo fulani.

Namba tisa. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba tisa?

²⁰⁵ Mama huyu hapa? Vema. [Dada huyo anasema, "Namba nane."—Mh.] Namba nane. Vema.

²⁰⁶ Namba tisa, ni nani aliye na kadi ya maombi namba tisa? Angalieni kote. Mtu fulani huenda akawa ni kiziwi. Namba tisa. Namba tisa. Walitoka nje? Angalieni kote kwenye ninii zenu. . . Tuseme, mtu yeyote aliye na kadi ya maombi mkononi mwao, angalieni kote. Labda ni mtu fulani asiyeweza kusimama. Kadi ya maombi namba tisa. Hatutaki kumkosa mtu yeyote.

²⁰⁷ Huyu mama *hapa* ana kadi namba tisa? [Mtu fulani anasema, "La, bwana. Kumi na nne."—Mh.] Angalieni.

²⁰⁸ [Mtu fulani anasema "Ishirini na sita. Ishirini na sita."—Mh.] La. La. Hiyo ni—hiyo ni kule juu kabisa.

²⁰⁹ Namba tisa. Hutakuja tu, isipokuwa namba yako imeitwa, tafadhali. Namba tisa.

²¹⁰ Ninamjua mama huyu. Bibi Ford, unayo kadi ya maombi namba tisa? Mtu fulani aone. Labda hawezi kusikia. Gene, waweza kushuka huku, kwa dakika moja tu, ukalishughulikie?

Ndugu Fred, njoo hapa ukamsaidie Billy, kwa dakika moja. Vema.

211 Namba kumi, ni nani aliye na namba kumi? Namba tisa, namba kumi?

212 Kila mtu yuko wapi? Vema. Tutaanza na hizi, basi, tuzipate hizi. Vema.

213 Sasa, ni wangapi wenu hapa kwenye mstari wa maombi wanaijua mimi? *Wewe* unaijua, na *yeye* anaijua. Vema.

214 Ni wangapi hapo kwenye kusanyiko ambao hawanijui mimi? Nami siwajui. . . Unajua kwamba mimi sijui shida yako, na hata hivyo wewe ni mgonjwa? Inua mkono wako. Vema. Vema.

215 Sasa, ninyi msionijua mimi, wala mimi siwajui, ninawatakeni mfanye hili. Ninawatakeni mwangalie juu huku, na mfanye kama yule mwanamke alivyofanya, wakati tukiwa tu na mstari huu mdogo wa maombi.

216 Sasa, angalieni. Hao watu ni wagonjwa. Sioni viwete wowote, lakini—lakini watu hawa ni wagonjwa. Sasa, kama wanahitaji uponyaji, vema, kuna Jamaa mmoja anayeweza kuwaponya, huyo ni Yesu Kristo, Mtu mmoja. Sasa, Yeye anawezaje kulifanya? Analifanyaje? Kwa sababu unaamini kwamba amelifanya, kwamba unaamini kwamba Yeye amelifanya. Sasa, kama Yeye yu hai, basi Yeye angali ni mponyaji. Hiyo ni kweli? Inueni mikono yenu. Kama angali hai, Yeye angali ni mponyaji. Vema. Basi, kama anaweza kuwathibitishia ya kwamba Yu hai, hapa usiku wa leo, kama anaweza kujithibitishia Mwenyewe.

217 Sasa, hawezi kuwa hapa katika umbo la mwili, kwa sababu mwili Wake umeketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Na wanajua ya kwamba Roho Mtakatifu, aliyekuwa ndani Yake, amerudi hapa sasa akifanya kazi zile zile alizofanya wakati alipokuwa ndani Yake, yale Yeye aliyosema. Vema. Sasa, kama Yeye atafanya kazi zile zile alizofanya, ndani yetu.

218 Sasa, ninyi msio na hizo kadi za maombi, wala hamnijui mimi, na uliina mkono wako, angalia upande huu, na useme, “Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe uko hapa ndani, nami ninataka kuligusa vazi Lako. Kwa kuwa Biblia ilisema ya kwamba Wewe, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Mimi ni mgonjwa, na ninahitaji maombi. Nami ninataka kuligusa vazi Lako. Basi, Wewe nena kupitia Ndugu Branham tu kuniambia la kufanya.” Fanya—fanya tu hivyo, uone kama Yeye yuko hapa, ama hayupo.

219 Ni nani wa kwanza katika mstari wa maombi? Vema. Je, ma-. . . Huyu, mama kwenye hiki kiti hapa? Vema. Vema.

220 Jambo la kwanza, na—naamini si—sikujui, sidhani. Hatufahamiani. [Dada huyo anasema, “Ndiyo,

hatufahamiani.”—Mh.] Hatufahamiani. Vema. Sasa, huyu hapa mwanamke ambaye simjui. Sijui chochote kumhusu. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye ni mgeni kwangu.

²²¹ Nasi tuko hapa kama mfano, kama tu ilivyokuwa katika Biblia. Hapa mwanamume na mwanamke wanakutana, kama vile Yohana Mtakatifu 4, mkitaka kuisoma. Yesu alikutana na yule mwanamke kisimani. Na Yeye kamwe hakuwa amemwona, wala huyo mwanamke hakuwa amemwona Yeye, hapo kabla.

²²² Kwa hiyo akasema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake.

²²³ Naye akasema, “Si kawaida kwa Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho. Hatuna uhusiano.”

Akasema, “Nenda kamwite mume wako, mje hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

²²⁴ Kasema, “Hiyo ni kweli. Unao watano. Yule unayeishi naye siye wako.”

²²⁵ Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Sasa, tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

²²⁶ Ndipo akakimbia, akauambia mji wote. “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya,” ama kitu fulani kumhusu. “Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

²²⁷ Vema, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi katika siku hiyo, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hivi si ingekuwa vile vile leo hii kama ilivyokuwa wakati huo basi? Hivi hatafanya jambo lile lile?

²²⁸ Ni wangapi wenu kwenye jengo hili, mwenye dhambi, au asiye, angeliamini kama Yeye angelifanya vivyo hivyo? Hebu tuuone mkono wako.

²²⁹ Sasa huu hapa mkono wangu. Nijuavyo mimi, sijawahi kumwona mwanamke huyu maishani mwangu mwote. [Dada huyo anasema, “Asante, Yesu.”—Mh.] Amesimama hapa, akisema, “Asante, Yesu.” Huenda akawa ni Mkristo. Huenda akawa siye.

²³⁰ Kunao watu wengi wanaosema, “Asante, Yesu,” wasiojua chochote kumhusu Yeye. Wengi wao. Mnaona? Akasema, “Wengi watakuja Kwangu, Siku hiyo, wakisema, ‘Bwana, Bwana.’ Hata sikuwajua kamwe,” Yeye akasema.

²³¹ Sasa, kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye yuko hapa miongoni mwetu, ikiwa ninaweza kujinyenyekeza mbele Zake, kujitolea Kwake, basi angefanya kazi kupitia kwangu kama tu alivyofanya na ninii Yake. . . Mungu atatenda kazi kupitia kwangu kama alivyofanya kupitia kwa Yesu, pamoja na yule mwanamke kisimani? Hiyo ni kweli? Sasa, sisi

hapa, sote wawili kamwe hatujawahi kuonana. Ingewafanya ninyi nyote kuamini? Ingeweza kuitia nguvu imani yenu? Basi kama Yeye yuko hapa, kama Yu hai, basi Yeye angali ni Mwokozi wako, angali ni mponya wako. Hiyo ni kweli? Sasa tuone kama atafanya.

²³² Sasa, Mungu, hili liko mikononi Mwako sasa. Yaliyobaki ni Yako, kwa kuwa tunajua ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya mambo haya. Inabidi yatoke Kwako. Tafadhali, Baba, usiku wa leo, kwa manufaa ya watu wanaoketi hapa, kwa ajili ya utukufu wa Injili, na lifanyike, usiku wa leo, Baba, ili watu waweze kujua ya kwamba Wewe ungali ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

²³³ Pia jalia gi—giza ambalo huenda likawa katika baadhi ya mioyo yao sasa, pasipo kujua, wakibahatisha, wakishangaa, kama Wewe utakuja tu na kuiangaza Nuru, jalia waone Njia hiyo, basi, na waingie ndani Yako. Wakiwa ni wagonjwa, jalia waponywe. Kama wamepotea, jalia waokoke. Tutaona njia ya kurudi ufukoni, wakati Mwana atakapochomoza. Tujalie, Bwana. Jalia “Mwana wa haki ainuke sasa na uponyaji katika mbawa Zake,” na kuutandaza Utu Wake mkuu juu ya mahali hapa. Lijalie, Baba. Tunaomba hayo kwa utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²³⁴ Ninawatakeni mwe na kicho, kwa kuwa tunatambua hatuwezi. . . Huku sio kuigiza kanisa. Huku ni kuuita Uwepo wa Mwenyezi Mungu uingie kwenye jengo hili.

²³⁵ Sasa mnaona mahali ninaposimama? Kuna watu mia moja na hamsini hapa. Nimesema hili mbele ya makumi elfu, na mia moja elfu, na kadiri ya laki tano, wakati mmoja, mahali walipokuwa wameketi kule pamoja na wakana-mungu, wasioamini, makafiri, washika nyoka, na kadhalika. Yeye hatashindwa.

²³⁶ Sasa, hana budi kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu wa Biblia, ama Yeye si Mungu wa Biblia. Na iwapo Yeye ni Mungu wa Biblia, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, kama anaweza kumwambia mwanamke huyu kilichomleta hapa. Sijawahi kumwona. Ama, kumwambia jambo fulani analojua sijui kitu kulihusu. Iwapo anaweza kumwambia kilichomleta hapa, kama alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, kama anaweza kumwelezea kitu fulani anachojua. Iwapo hata simjui, wala yeye hanijui mimi, basi sisi hapa tumesimama hapa kwa mara ya kwanza maishani, hakika hilo lingekutikisa sana, hata ukungu wote ungekuondokea. Na alijalie, ndilo ombi langu.

²³⁷ Sasa, huyu mama aliye hapa kuombewa, ninataka kila mmoja aamini sasa. Sasa, bila kumjua huyu mama, ningetaka tu kuongea naye kwa dakika moja tu, kama Bwana wetu alivyomfanyia yule mwa—mwanamke ki—kisimani, ili tu kuwasiliana na roho yake.

238 Sasa, labda sisi...Kamwe hatujakutana awali, bali hata hivyo Bwana anakujua, Naye ananijua. Kama anaweza kuniambia kile kilichokuleta hapa, kuniuliza, kitu fulani ambacho—ambacho unakijua. Wala sijui chochote kukuhusu wewe.

239 Sasa, kama Yeye alikutuma hapa, na kunileta hapa, labda ninaweza kukuelezea, ama Yeye anaweza kunena kupitia kwangu na kuniambia kilichokuleta hapa jukwaani, ingekufanya umwamini? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, kingenifanya.”—Mh.] Kingekufanya uamini? Sasa, ninaona.

240 Nalo kusanyiko lilisema wangeamini. Sasa, sisi hapa, tayari kwa jambo fulani kutukia, kama Mungu angali ni Mungu. Jambo lile lile ambalo Yesu Kristo alifanya!

241 Ninaweza kumwona huyu mama sasa. Anataka niyaombee macho yake. Ana tatizo fulani na macho yake. Sasa, hiyo haikuwa ni kubahatisha. Hiyo ni kweli. Macho yake yanafifia, naye anataka kuombewa, macho yake. Hiyo ni kweli. Hiyo ni... Iwapo hiyo ni kweli, watikisie lesa hiyo, dada.

242 Sasa, sijawahi kumwona hapo kabla, maishani mwangu. Ni kitu gani kilichofanya hayo? Ni kitu gani kilichofanya hayo? Anaonekana kuwa ni mtu mzuri. Mnafikiri nilibahatisha hilo? Vema, tutaona.

243 Sasa, mama, kusudi mashaka yote yaondolewe kutoka kwenye kanisa hili, tangu sasa na kuendelea, ili kwamba wakati Ndugu Ruddell anapohubiri kwamba, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” kwamba ijulikane, na mimbara hii, ya kwamba Kristo Yesu aliudhihirisha utukufu Wake na kuthibitisha kuwa ndivyo ulivyo:

244 Sasa, naam, ninaona yeye... Macho yake yanaharibika. Ni uastigmati kwenye macho yake. Halafu, jambo lingine, ana tatizo fulani. Ana ninii... Alifanyiwa upasuaji wa namna fulani. Huo umesababisha tishu kubwa ya kovu. Hatoki kwenye mji huu. Wala hatoki kwenye mkoa huu. Anatoka Kentucky. Hiyo ni kweli. Naye ana binti anayetaka aombewe. Msichana mdogo, yapata umri wa miaka minane ama kumi. Anataka maombi kwa ajili ya binti huyo kwa sababu huyo binti anatarajia kufanyiwa upasuaji. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

245 Angalieni kama hiyo ni kweli ama si kweli. Hiyo ilikuwa ni kweli, mama? Iwapo hiyo ni kweli, itikise lesa hiyo tena, kwa watu. [Dada huyo anasema, “Asante, Yesu. Yeye ana umri wa miaka sita tu.”—Mh.] Ni msichana mdogo. Vema.

246 Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Iwapo Mungu... Hapa, nitakuonyesha jambo jingine. Huyu hapa mwanamume anakuja, amesimama karibu nawe, huyo ni mumeo. Ameketi moja kwa moja nyuma hapa. Hiyo ni kweli. Yeye pia anahitaji uponyaji. Ana baridi yabisi. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Camper. Hiyo ni kweli. Nawe unatoka

Kentucky. Rudi huko chini Kentucky, na upokee. . . Chukua lesa hiyo ukaiweke juu ya huyo mtoto. Amini kwa moyo wako wote, usifanyiwe upasuaji. Amina. Unaamini kwa moyo wako wote?

247 Hiyo ni karibu ensaiklopedia nzima ya maisha ya huyo mwanamke. Ninaishika mikono yangu, kamwe sijawahi kumwona hapo awali, maishani mwangu. Kweli.

248 Sasa, mnaona, yeye aligusa nini? Alifanya nini? Alingusa yule Kuhani Mkuu. Alingusa Yule anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Amina.

249 Sasa, uponyaji ni ushahidi wa Mungu mwenyewe, Utukufu Wake Mwenyewe. Vema.

250 Wewe, ninaamini wewe ni mgeni kwangu. Siamini ninakujua. Mungu anakujua. Iwapo Mungu atanifunulia shida yako ni nini, ama kile unachotaka; kama ni maradhi, mambo ya nyumbani, ama chochote kile; utaamini kwa moyo wako wote, sivyo, mama?

251 Sasa, huyu hapa mama mwingine nsiyemjua, wala yeye hanijui mimi. Hatufahamiani kabisa. Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, maishani. Lakini, kama Roho Mtakatifu anaweza kuja, Uwepo uingie hapa sasa na kutwambia jambo fulani kumhusu mwanamke huyu!

252 Sasa, kumponya, nisingeweza kufanya hivyo. Yeye. . . Mungu alifanya hivyo hapo alipokufa Kalvari. Iwapo yeye ni mwenye dhambi, siwezi kumwoko. Kwa sababu, Yesu alifanya hivyo pale. . . Hilo limekwisha tayari. Lakini Yeye anaweza kuja katika Uwepo wa Utu Wake, kuonyesha ya kwamba Yeye angali hai, na kazi Zake zingali ni halisi, kulifanya halisi kwetu, kama tunaweza kuliadini.

253 “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.” Kama unaweza tu kuamini sasa. Mwamini Mungu. Usitie shaka.

Sasa, mtu fulani anajisikia vizuri sana. Ninii tu, hilo ni sawa.

254 Nilikuwa nikishuka kupitia mkoa wa Kentucky, hivi majuzi, nikamsikia mtu akipitia vichakani, akipiga mayowe. Nikasema, “Hivi mtu huyu. . . Ana shida gani?”

Kasema, “Yeye amelewa tu na anajisikia vizuri.”

255 Ndivyo ilivyo na mtu huyu, ila amelewa kwa kinywaji kingine. Amelewa tu na anajisikia vizuri. Hiyo ni kweli. “Kwa hiyo msilewe kwa vileo vikali, bali mlewe kwa Roho,” ilisema Biblia.

256 Sasa, mwanamke huyu hapa, akiwa ni mgeni, iwapo Mungu anaweza kumwambia shida yake ni nini, ama jambo fulani kumhusu, ambalo anajua ya kwamba sijui, na awe shahidi, atajua kama ni kweli, au sivyo. Hiyo ni kweli, mama? Ingekusaidia kama Mungu akifanya hivyo? Sasa, kukuponya,

dada, kama ningeweza kufanya hivyo, ningekuponya, bali siwezi. Mimi ni mwanadamu tu.

²⁵⁷ Lakini huyu mama yupo hapa apate kuombewa. Ana ugonjwa wa ugumu unaoota kwenye nyongo. Hiyo ni kweli. Pia ana kisukari. Hicho ndicho unachotaka kiombewe, sivyo, mama? Iwapo hiyo ni kweli, inua mkono wako, kusudi watu waweze kuona. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Hilo lingeweza kukusaidia? Lingekusaidia? Basi, Bibi Johnson, rudi ukaketi kitini mwako, na uponywe, kama unaamini, katika Jina la Bwana Yesu.

²⁵⁸ Kama huwezi kuamini, sijui kuna shida gani. Kuna shida fulani. Hivi hamwoni? Mwanga wa Mwana unamulika. Hilo ni jambo lile lile ambalo Yesu Kristo alifanya.

²⁵⁹ Ninamfahamu mtu huyu. Nilikuwa... Mama mkwe wake yuko hapa. Na—nami ninamjua mke wake. Sijamwona kwa muda mrefu, mrefu sana. Jina lake ni James Morris. Ila sijui kilichomleta hapa. Sijui ana shida gani. Sijamwona Jim kwa muda mrefu sana. Lakini mimi... Alinijua nilipokuwa mvulana mdogo. Lakini, Jim, kama Bwana anaweza kunifunulia kilichokuleta hapa, utalikubali, kama ni...uamini, basi, utapata ulichoomba? [Huyo Ndugu anasema, “Amina.”—Mh.] Uko hapa kwa ajili ya mwana. Huo ni ugonjwa wa kurukwa na akili. Unaamini ataponywa? [“Amina.”] Nenda ukaliamini, basi. Amini tu, kwa moyo wako wote. (Nafikiri sina budi kuwatembelea, Ndugu Jim.)

²⁶⁰ Ninamjua mama huyu. Yeye ni mke wa rafiki yangu mpendwa sana. Jina lake ni Himmelheber. Nilikuona kwenye duka, hapa, si muda mrefu uliopita. Sina fununu una shida gani. Ninakujua. Ninamjua mume wako. Mimi na mume wako tulilelewa pamoja, kama wavulana. Naye alisoma, ninaamini, tabibu wa maungo, kuwa tabibu wa maungo. Hiyo ni kweli. Nami...kujua tu shida yako. Lakini kama Bwana atanifunulia...

²⁶¹ Sasa, Bibi Himmelheber, kwa ajili ya—ya—ya—ya Gilbert, na dada yake niliye kuwa nikiambatana naye, kama kwa—kwa ajili yao, kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo, bali siwezi. Lakini Yeye atakuponya, kama utaamini sasa. Na endapo Yeye atakujalia kujua ya kwamba—ya kwamba... Hakika, ninajua jina lako. Nami nimekujua kwa muda mrefu, ila sijui una shida gani. Ikiwa Mungu ataniambia shida yako, utamwamini Yeye, kwa ajili ya uponyaji wako? Yabisi kavu ndiyo shida yako. Ninaona umeshupaa, ukijaribu kutoka kitandani, asubuhi. Hiyo ni kweli kabisa. Vema. Rudi nyumbani ukapokee uponyaji wako, Bibi Himmelheber. Bwana Mungu akupe afya. Amini kwa moyo wako wote.

²⁶² Bwana awabariki. Unaamini kwa moyo wako wote? Mwaminini Mungu. Vema.

263 Huyu hapa mama. Angalia hapa, dada. La, simjui mwanamke huyu. Nadhani hatufahamiani. Lakini Mungu anatumjua, hiyo ni kweli? Tulizaliwa, tukiachana kwa miaka kadhaa, bali huu ndio wakati wetu wa kwanza kukutana, nijuavyo mimi, ama ujuavyo wewe. Huu ndio wetu wa kwanza. Mnaweza kumwona akitikisa kichwa chake. Hiyo ni kweli. Hii ndiyo mara ya kwanza niliyopata kumwona huyu mwanamke, maishani mwangu. Bali—bali Mungu anatumjua sote wawili. Alitujua tangu tulipokuwa watoto. Alitujua. Alitujua kabla ulimwengu haujaumbwa. Alijua tungekuwa tumesimama papa hapa, usiku wa leo.

264 Alijua tukio hili lingetukia, kabla hapajakuwapo hata na a—atomi wala molekuli. A—alijua hilo, Yeye, kwa sababu alikuwako. Hana kikomo. Alijua kila kitu kabla ulimwengu haujapata kuumbwa. Alijua kila kitu kilichowahi kutukia. Yeye alijua kila kijidudu, kila wakati kinapolipepesa jicho lake. Anajua kila kitu, maana Yeye hana kikomo. Mnaona? Wala huwezi kuwekea mipaka kisichokuwa na kikomo kwa chochote. Yeye ni ninii tu. . . Yeye ni. . . Ni ukamilifu tu wa ukamilifu, unaokaa mle ndani. Amewasili tu. Hivyo tu. Mnaona?

265 Sasa, ikiwa Yeye anaweza kuniambia shida yako ni nini, basi utaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anasema, “Bwana!”—Mh.] Utaamini, moyo wako wote? [“Ndiyo.”] Vema.

266 Unaugua ugonjwa wa moyo ambao unataka uombewe. Moyo. Hiyo ni kweli.

267 Sasa, jambo lingine moyoni mwako, hata hivyo. Unaona, nilishika hilo. Unaona? Uliwazia, “Hivi yeye atanirudisha kabla hajasema jambo hili?” La. Nitakwambia. Uko hapa kwa ajili ya mvulana mmoja, mwanao. Hiyo ni kweli. Naye huyo mwana hayupo hapa. Mwana huyo yuko Ohio. Yuko katika hospitali ya TB, akiwa na TB. Wala hajaokoka. Nawe unaiombea nafsi yake, na uponyaji wake. BWANA ASEMA HIVI.

268 Ninawapa changamoto mlichunguze hilo kabisa, muone kama hilo ni kweli, ama si kweli. Hiyo ni kweli. Sivyo, mama? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana. Amina.”—Mh.] Ni ukweli. [“Ndiyo.”] Vema. Siwezi kuponya. Utaamini? [“Ndiyo, bwana.”] Basi nenda ukapokee. Kama tu vile ulivyoamini, hicho ndicho hasa utakachopokea. Nenda, katika Jina la Bwana. Amina.

269 Mnaamini kwa moyo wenu wote? Mnaona? Yeye, ninii. . . Vema, Nuru inamulika. Tunajua mahali tulipo sasa. Tuko katika Uwepo wa Bwana Yesu.

Mnasema, “Anasoma mawazo yenu.”

270 Vema. Hata sitamwanguka mama huyu. Weka mkono wako juu ya wangu, mama. Kama Bwana ataniambia huku, nikiangalia *huku*, shida uliyo nayo, utaamini? Na kuamini ya kwamba utaponywa? Uko mgongoni mwako. Hiyo ni kweli.

Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako juu kutoka kwa wangu. Nenda, ukaponywe. Yesu Kristo anakuponya. Unaona? Vema.

271 Yeye ni—Yeye ni Bwana Yesu tu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Vema.

272 Mtu huyu anayekuja, unataka kuponywa yabisi kavu? Unaamini kwamba Mungu atakuponya? Rudi ukapate afya. Hivyo ndivyo tu ilivyo rahisi. Liamini tu. Rudi kitini mwako ukaseme, “Ninaamini kwa moyo wangu wote, kwa akili yangu yote.” Utaona. Amini tu kwa moyo wako wote. Usitie shaka. Vema, bwana.

273 Mwanamke huyu hapa, hakika, mnaona anatetemeka. Yuna ugonjwa wa kupooza. Labda kuna shida nyingine. Hebu tuone. Naam, bwana. Ana kisukari. Unaamini Mungu atakuponya hicho kisukari, mama?

274 Bwana Mungu, tunakilaani kitu hiki kiovu, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia aponywe. Amina.

Rudi kitini mwako ukapone, dada.

275 Unaamini kwa moyo wako wote?

276 Na wewe je, unayeketi hapo? Unaamini? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Kuna ninii...Kama unaweza kuamini.

277 Ninyi msio na kadi ya maombi, ninyi mlio—mlio wagonjwa na wahitaji, mwaminini Mungu. Mnaweza kuliadini. Vema.

278 Ulimleta mvulana huyo apate kuponywa. Uko mgongoni mwake. Hiyo ni kweli. Yeye ni kiwete. Unaamini unaweza kumrudisha huko chini Arkansas, apate kuponywa, na awe mzima? Unataka kuachana na hizo sigara, na kusema, “Nitaziacha,” na uwe...na—na kumtumikia Bwana na kufanya yaliyo mema? Utafanya hivyo? Vema. Vema. Basi nenda, ukaweke mkono wako juu ya mtoto huyo sasa, unaposimama pale. Bwana Mungu wa Mbinguni na amponye mtoto huyu. Na kumfanya...

Ninakusahi uamini.

279 Yupo mama anayeketi hapa, akiangalia huku ameinamisha macho yake, akiangalia, akiniangalia mimi. Una shida na mguu wako. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ungeniamini? Bibi Worley. Vema, bwana, hiyo ni kweli kabisa. Kamwe sijawahi kukuona maishani mwangu. Huyu ni mume wako anayeketi nyuma yako hapo. Yeye ni mhubiri. Sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini hiyo ni kweli.

280 Unaamini Mungu anaweza kuniambia una shida gani, bwana? Una mahali usoni mwako, hujui kama ni kansa, hujui ni nini. Una henia, pia. Hiyo ni kweli. Unataka kuponywa. Hiyo ni kweli, Bw. Worley. Vema. Unaamini kwa moyo wako wote? [Huyo ndugu anasema, “Naam.”—Mh.] Basi nenda ukapokee uponyaji

wako, katika Jina la Bwana Yesu. Jambo ndilo hilo. Hiyo ni kweli.

²⁸¹ Vipi kuhusu macho yako? Unaamini Mungu atakuponya, huko nyuma, unayeketi hapo ukiniangalia? Vema. Kama unaamini kwa moyo wako wote. Kuwa tu na imani katika Mungu, hayo tu ndiyo yakupasayo kufanya.

²⁸² Loo, jamani! Inatendeka kila mahali, sasa, kama unaweza tu kuamini. Inakuwa nyingi sana humu ndani sasa, kila mtu anajaribu kuamini. Sasa mnaamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu? Unaamini Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele?

²⁸³ Sasa, kuna mtu hapa asiyemjua kama Mwokozi wako, nawe unataka kuokolewa? Ungetaka kufanya hivyo? Kamwe hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, nawe ungetaka kuja na kuwa katika Kristo, uweze kuwa mwaminio? Inua mkono wako, kama ukisema, “Ningetaka . . .” Mungu awabariki. Njoni huku madhabahuni, sasa hivi.

²⁸⁴ Tupe sauti kidogo kwenye piano hiyo hapo, kwa dakika moja tu, kabla hatujamalizia.

²⁸⁵ Ninawaalika, njoni huku, madhabahuni hapa. Njoni papa hapa mkapige magoti. Jambo ndilo hilo, kijana. Simama moja kwa moja. Njoo huku, msichana mdogo. Wewe ambaye . . . Mwangalie mvulana huyu mdogo. Hiyo inapaswa kuwa ni aibu kwa wengine. Unataka kwenda kule, mbele? Unataka kumkaribia Yeye? Njoo moja kwa moja sasa. Njoo moja kwa moja huku. Amina. Njoo moja kwa moja sasa katika Uwepo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli, ndugu. Njoo huku, sasa. Mwaweza kuja hapa juu na kupiga magoti, kabla ibada ya uponyaji haijaendelea. Njoni moja kwa moja hapa juu sasa mkaponywe nafsi, kisha mwangalie kitakachotukia. Njoni katika Kristo.

²⁸⁶ Yeye ndiye Njia, Kweli, Nuru. Hakuna mtu ajaye, nje ya Yeye. Aisee, Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mluteri, hata uwe nani, ambaye hujampokea Roho Mtakatifu, sasa ndio wakati wa kufanya hivyo. Njoni huku sasa, na mwingie ndani ya Kristo. Mtashangazwa na jambo Hili. Hamtajua jinsi ya kulishika Hilo. Hamtalielewa, isipokuwa mumpokee Roho Mtakatifu. Njoni sasa.

²⁸⁷ Kama nimesema Kweli, Mungu alizungumza nami. Mungu alinena kupitia kwangu. Nimewaambia Kweli. Yeye ndiye Njia pekee. Ndiye Msingi pekee. Ndiye wokovu pekee. “Hakuna wokovu katika jina lingine lolote lililotolewa chini ya Mbingu, ila katika Jina la Yesu Kristo.” Hivi hamwezi kuja, mkampokee sasa?

²⁸⁸ Ni wangapi waliorudi nyuma walio huko nyuma, wangetaka kuja huku, wakapige magoti sasa? Wewe ambaye umerudi nyuma na ulimwacha Mungu, je, ungetaka kuja sasa? Njoo huku. Hii ndiyo ile saa.

289 Sasa angalieni. Kama ukiikataa hii, sijui, sijui kama kunalo, kwa yeyote wenu, tumaini lolote kwako, ama hakuna. Sasa, sisemi kwa sababu nimesimama hapa. Bali ninawaambia, enyi marafiki, Mungu anaweza kufanya nini zaidi? Huu ndio wakati. Hii ndiyo ile saa Mungu anazungumza na watu.

290 Hiyo ni kweli, dada. Hiyo ni kweli, akina dada. Njoni moja kwa moja. Hii ndiyo ile saa. Huu ndio wakati wenu. Kamwe hutakuwa karibu zaidi na Yeye, mpaka utakapokufa na kwenda Mbele Zake. Yeye yuko papa hapa, akijithibitisha Mwenyewe kuwa hai. Hivi hutakuja?

Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!

Hivi nilivyo, bila hoja moja,
Ila kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa ajili
yangu,
Nami nijapo, nitaamini,
Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!
Hivi nilivyo, na bila kungojea
Kuiondolea nafsi yangu ninii moja . . .

291 Wana waa moja jeusi, ni kutokuamini. Njoni. Jambo ndilo hili.

Wewe, ambaye Damu Yako inaweza kusafisha
kila doa,
Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Na- . . .

292 Ungewezaje kumkataa, akiisha kuja kupitia kwenye Maneno, akaja Binafsi, akakujulisha ya kwamba Yeye yuko hapa, akikuzungumzia, akikuzungumzia sasa? Sauti hiyo ndogo inakuzungumzia. Hiyo ni Mungu. Yeye anakutaka uje. Hatuna muda mrefu zaidi kuwa hapa, enyi marafiki. Tunaondoka hapa. Hivi hutakuja na kupiga magoti pamoja na kundi hili la watu? Useme, "Mungu, unirehemu. Sasa ninataka kumkubali Kristo. Ninataka kuzaliwa mara ya pili. Ninataka kujazwa na Roho Mtakatifu. Ninataka kitu kilicho halisi. Ninataka kuwa halisi."

293 Njoni, sasa hivi, kuyazunguka madhabahu, tunapoimba kifungu hiki kinachofuata. Hivi utakuja sasa wakati tukija?

294 Sasa, baadhi yenu Wakristo wazuri njoni huku, karibu pamoja nao. Baadhi yenu mlio wagonjwa njoni, pigeni magoti, pia. Baadhi yenu ninyi watu mlio Wakristo, njoni huku mkapige magoti pamoja na hawa, tunapoomba.

. . .kupokea,
Utanikaribisha, unisamehe dhambi, unifariji.
Kwa sababu . . .

Ambatana nao, ewe mwenye dhambi. Ambatana nao, wewe.

. . .naamini,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja!

Njoni moja kwa moja humu . . .? . . .

Hivi nilivyo, na bila kungojea
 Kuiondolea nafsi yangu doa moja jeusi,
 Kwako Wewe, ambaye Damu Yako inaweza
 kusafisha kila waa,
 Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu . . .

295 Utakosa baraka usipokuja.

Jinsi tu nilivyo, Wewe utanipokea,
 Utanikaribisha, unisamehe, unisafishe,
 unifariji;
 Kwako Wewe ambaye Damu Yako inaweza
 kusafisha kila waa,
 Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!

296 Vema. Hebu kanisa zima sasa mwinamishe vichwa vyenu. Kila mmoja, katika maombi, waombeeni watu hawa waliyozunguka madhabahu, kila mmoja.

297 Kila mtu hapa madhabahuni, sasa, umekuja juu ya msingi wa damu iliyomwagika. Umekuja hapa kumpokea Roho Mtakatifu. Umekuja kusamehewa dhambi zako; Mungu, aliye wa haki na yuko tayari.

298 Kutakuwako na maji yakingojea. Mnaweza kuja kwenye kidimbwi, kesho, mkabatizwe, huko kanisani, ikiwa mchungaji anataka kuwaleta kule.

299 “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”

300 “Petro alipokuwa akisema Maneno hayo, Roho Mtakatifu aliwashukia wale waliolisikia, kwa sababu waliwasikia wakinena kwa lugha.”

301 Mungu wa Mbinguni, Yule aliyekuwa pamoja na mitume, Yule aliye Mungu milele, Yeye yuko hapa usiku wa leo.

302 Sasa kila mtu na ainame katika maombi. Kila mtu ipaze tu sauti yako na kuomba, wakati mchungaji akituongoza.

Ndugu Ruddell. Vema. 

60-0604 Twende Kwa Nani?
Gospel Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org